الإمام
زَين العَابِدِين عليه السّلام
وبناء الإنسان

IMAM ZAINUL ABIDIN (A.S) NA KUMJENGA BINADAMU

Kimeandikwa na:
Sheikh Dkt. Abdullah Ahmad Al-Yousif

Kimetarjumiwa na:
Amiri Mussa

Imam Zainul Abidin (a.s.)

na

Kumjenga Binadamu

الإمام زَين العَابِدِين عليه السّلام وبناء الإنسان

Kimeandikwa na:
Sheikh Dkt. Abdullah Ahmad Al-Yousif

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Amiri Mussa

الإمام زَين العَابِدِين عليه السّلام وبناء الإنسان

تأليف
الشيخ الدكتور عبدالله أحمد اليوسف

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

©Haki ya kunakili
imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978–9987-17-140-8

Kimeandikwa na:
Sheikh Dkt. Abdallah Ahmad Al-Yousif

Kimetarjumiwa na:
Ustadh Amiri Mussa

Toleo la kwanza: Mei, 2021
Nakala: 2000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
S.L.P.- 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu:+255222110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv.co.tz
Vitabu mtandaoni: www.alitrah.info/ebooks/

ILI KUSOMA QUR'ANII MUBASHARA
KWA NJIA YA MTANDAO,
TEMBELEA www.somaquran.com

YALIYOMO

Dibaji....6
Neno la Mchapishaji....7
Utangulizi....9
Imam Zainul Abidin (a.s.) na malezi kwa njia ya dua....12
Sahifatul-Sajjadiya na malezi kwa njia ya dua....15
Athari za dua....20
Masharti ya kujibiwa dua....21
Kumjua Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla)....22
Kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla)....22
Kuhudhurisha moyo....22
Chumo la halali....24
Sifa za dua....24
Kuangalia nyakati tukufu....25
Vizuizi vya dua....26
Kutenda mambo ya haramu na yaangamizayo....26
Kuwadhulumu waja....26
Kutoamrisha mema na kukataza maovu....27
Kula vya haramu....28
Maslahi ya mja....28
Aina za dua zenye kujibiwa....29
Dua ya mzazi kwa mwanawe....29
Dua ya mdhulumiwa kwa aliyemdhulumu....29
Dua ya muumini kwa muumini mwenzake....30
Dua ya msomaji Qur'an na mwenye kudumisha kuisoma....31
Imam Zainul Abidin (a.s.) na suala la kuwaacha huru watumwa....31
Imam Zainul Abidin (a.s.) na wafanyakazi wake....32
Muamala wa kibinadamu wa Imam Zainul Abidin (a.s.) na watumwa....35
Kuwaelimisha watumwa....35
Kuoa vijakazi na kuzaa nao....35
Kuwasamehe watumwa....38
Kuwaacha huru watumwa....40

Imam Zainul Abidin (a.s.) na kuwajali mafukara.....42
Kuamiliana na mafukara kibinadamu.....42
Kuwakirimu na kuwatukuza mafukara.....42
Kuwafanyia upole mafukara.....42
Alikataza kuwarudisha waombaji.....43
Kuwalipia madeni.....44
Kulisha chakula mwaka mzima.....45
Kuzihudumia familia mia moja.....45
Kuwafanyia tahfifu mafukara.....45
Imam Zainul Abidin (a.s.) na Waraka wa Haki.....47
Imam Zainul Abidin (a.s.) na kuasisi haki za binadamu.....48
Yaliyomo katika Waraka wa Haki.....49
Haki za muhimu zaidi.....50
Waraka wa Haki na uadilifu wa kijamii.....52
Rejea.....54

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمنِ الرَّحِيْمِ

DIBAJI

Kitabu hiki ni toleo la Kiswahili la taasisi ya Al Itrah Foundation. Chapisho lake limelenga kukidhi mahitaji. ya kiroho ya zama hizi pamoja na mbongo na fikra za Muislam. Taasisi imefanya jitihada kubwa kuweka chapisho hili la Kiswahili katika msingi wa haki na wenye kukubalika katika Uislam.

Unaombwa kwa Taadhima ukisome kitabu hiki katika malengo yaliyokusudiwa. Pia unaombwa kuwasilisha kwetu maoni yako huru juu ya chapisho letu hili, jambo ambalo tutashukuru sana.

Kutangaza ujumbe wa Uislam ni kazi ambayo inahitaji ushirikiano wetu sote. Taasisi inakuomba kuungana na kushirikiana kama ilivyoagizwa katika aya ya Qur'an:

قُلْ إِنَّمَا أَعِظُكُمْ بِوَاحِدَةٍ، أَنْ تَقُومُوا لِلهِ مَثْنَى وَفُرَادَى ثُمَّ تَتَفَكَّرُوا...

"Sema: Hakika ninawapa mawaidha kwa jambo moja tu, kwamba msimame kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, wawili wawili na mmoja mmoja kisha mfikiri....." (Surat Saba; 34:46.)

Na rehma za Allah ziwe juu yako.

Wako katika Uislam

Al Itrah Foundation
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
SMS: +255 778 300 140

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمنِ الرَّحِيْمِ

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni cha mafunzo juu ya dua na manufaa yake. Mwandishi wa kitabu hiki anatuletea mafundisho yanayopatikana katika dua na maana zake kutoka kwenye kitabu maarufu cha Imam wetu wa nne, Ali bin Husain Zainul Abidin (Imam Sajjad) kiitwacho, Sahifah al-Sajjadiyyah.

Tunaambiwa kwamba duaa ni silaha ya muumini. Hivyo, Imam Zainul Abidin (a.s.) baada ya masaibu ya Karbala alichukuwa jukumu la kufundisha na kuwasiliana na wafuasi wake kwa njia hii ya dua, na kwa hakika wafuasi wake walinufaika sana kutokana na dua zake hizi na zikawa kama ngao na ngome dhidi ya maadui wao. Kuanzia mwaka huo wa 62 Hijria mpaka sasa, Waislamu wote wanazisoma na kuzitumia dua hizi katika maombi na shida zao mbalimbali kwa Allah (Azza wa Jalla).

Mwandishi wa kitabu hiki anajaribu kuzitolea ufafanuzi dua hizi na kuwahamasisha Waislamu kuzisoma pamoja na dua nyingine tulizofundishwa na Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Maimamu wengine watoharifu (a.s.).

Nasi pia kama taasisi ya dini hii tukufu tunakiwasilisha Kitabu hiki kwa wasomaji watukufu ili nao wapate kunufaika na hazina hii iliyomo kwenye dua hizi. Kitabu Sahifah al-Sajjadiyyah ni hazina kubwa tuliyoachiwa na mjukuu huyu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwa hiyo, yafaa na muhimu sana kwa kila Mwislamu kuwa na kitabu hiki nyumbani mwake. Jambo la kufurahisha ni kwamba kitabu hiki sasa kinapatikana kwa lugha nzuri ya Kiswahili, na bila ya kusahau kitabu chake kingine kiitwacho, Waraka wa Haki za Binadamu (Risalatu'l-Huquq) ambacho pia utapata taarifa zake kwa ufupi ndani ya kitabu hiki.

Tunamshukuru ndugu yetu Ustadh Amiri Mussa kwa kutarjumi kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kutoka Kiarabu. Aidha, shukrani zetu ziwaendee wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine mpaka kuwezesha kitabu hiki kuchapishwa. Allah (Azza wa Jalla) awalipe wote malipo mema duniani na Akhera pia.

Mchapishaji
Al-Itrah Foundation

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمنِ الرَّحِيْم

Kwa jina la Mwenyezi Mungu,
Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

UTANGULIZI

Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) anasema:

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ

"Hakika tumemuumba mtu katika hali nzuri mno".[1]

Imam Ali bin Husein bin Ali bin Abi Twalib (a.s.). (38 Hijiria, -95 Hijiria) ni Imam wa nne katika Maimamu wa Ahlul-Bayt watoharifu, ambao Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) amewaondolea uchafu na kuwatakasa kabisa kabisa.

Hakika Zainul Abidin (a.s.) alidhihiri katika kipindi cha uimamu wake kama Imam wa Waislamu, na ambaye watu walikuwa wanarejea kwake katika masuala ya kidini, na hivyo alikuwa mnara wa elimu, mbainifu wa hukumu za kisharia, pia mfasiri wa Qur'an tukufu.

Na alikuwa mfano wa kuigwa wa hali ya juu katika ibada, kujinyima, takwa, na uchamungu mpaka akawa anaitwa Bwana wa wenye kusujudu, pambo la wenye kuabudu na Imam wa wachamungu.

Kwa hakika Imam Zainul Abidin (a.s.) katika uhai wake alikabiliwa na changamoto nyingi na mambo makubwa ya kumtia majonzi, na kubwa zaidi lilikuwa ni tukio la Karbalaa lenye kuhuzunisha na kuumiza mno, na yale yaliyofuatia baada ya tukio hilo ambayo yalimfanya Imam Zainul Abidin (a.s.) aishi katika kipindi kigumu na alikabiliana nayo kwa subira, kujitenga na hekima.

Kwa hakika Imam Zainul Abidin (a.s.) alichukua majukumu l a

1. Surat at-Tin: 95:4.

uimamu baada ya kufa shahidi baba yake Imam Husein (a . s.) kilikuwa ni kipindi kigumu katika nusu ya pili ya karne ya kwanza ya Hijiria, na akatekeleza jukumu lake la uongozi na dini pamoja na kuwa mazingira hayakuwa rafiki kwake na yalikuwa magumu mno.

Imam Zainul Abidin (a . s.) aliona umma unakabiliwa na hatari k u b w a, na iliyodhihirika zaidi ni yale yaliyoleta athari mbaya kutokana na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali zilizoletwa ambazo zilileta athari katika shakhsia ya mwislamu, na mwelekeo wa umma wa kiislamu.

Na jambo lingine ni mmomonyoko wa kidini na kitabia, na kuenea maovu na mambo ya haramu ambayo ni matokeo ya maisha ya anasa na ubadhirifu katika kuendekeza starehe za dunia na matamanio yake. Hayo na yanayofanana na hayo yaliwafanya watu washughulike na dunia zaidi na kuwaweka mbali na roho ya Uislamu na makusudio yake, na malengo yake makubwa.

Baada ya matukio ya kuhuzunisha ya Karbalaa, Imam Zainul Abidin (a.s.) alianza kutilia umuhimu suala la kumjenga binadamu na kumlea kwa malezi madhubuti ya kidini na kielimu kwa ajili ya kuandaa watu na wadau wa ujumbe ambao wataongoza umma na kusahihisha mwenendo wa makosa, pia kuchangia katika kueneza elimu na maarifa katika nyanja mbalimbali za kielimu.

Kwa hivyo Imam Zainul Abidin (a . s.) alitilia umuhimu mkubwa suala la malezi na elimu katika kumjenga mwanadamu, kwani hizo ni nyenzo katika kuujenga umma, kuufanya upate maendeleo na mwamko wa kimaarifa.

Na kitabu hiki kinaangazia kwa muhtasari baadhi ya mambo ambayo Imam Zainul Abidin (a . s.) a l i y a s i m a m i a, yakiwa ni mambo muhimu katika mchakato wa kumjenga mwanadamu, mambo ambayo aliyatilia mkazo mno, na hapa tunaeleza yale ya muhimu zaidi kama ifuatavyo:

1. Jengo la kiroho (malezi kwa njia ya dua)

2. Jengo la ubinadamu (kuwaacha huru watumwa)
3. Jengo la kiuchumi (kuwajali mafukara)
4. Jengo la haki (Waraka wa haki mbalimbali)

Na kwa hayo alilenga na kukusudia kujenga utu na shakhsia ya binadamu mwislamu kiroho na kimaanawi, kielimu, kifikra pamoja na kiuchumi, kwa namna ambayo yatawafanya wanadamu hao kushika majukumu na kutekeleza wajibu mkubwa mbalimbali, na stahiki za kidini na kielimu, hayo na yanayofanana na hayo yatawawezesha kubeba majukumu makubwa, kufanya kazi, kuhudumia jamii na kuendeleza ardhi.

Na hakika wamehitimu katika shule ya Imam Zainul Abidin (a.s.) wanazuoni wengi, wasomi na shakhsia adhimu katika nyanja mbalimbali za kielimu na maarifa miongoni mwa wale walioshiriki vikao vya kielimu na masomo yake, na kubobea katika bahari ya elimu yake na maarifa yake.

Na katika kuhitimisha.....ninamuomba Mwenyezi Mungu (azza wa jalla) akifanye kitabu hiki kiwe na uzito katika mizani ya amali zangu, na kininufaishe hicho katika akhera yangu Siku ambayo haitomfaa mtu mali wala watoto, isipokuwa mwenye kuja kwa Mwenyezi Mungu na moyo safi, kwani Yeye Mola manani aliyetukuka ndiye kusudio, lengo la matumaini, chemchem ya rehema na mwingi wa utoaji. Na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye kuombwa msaada.

Abdullah Ahmad AlYousif.
al-Qateef
Ijumaa- 8 Ramadhani 1438 Hijiria.
2 Juni, 2018

بِسْمِ اللهِ الرَّحْمنِ الرَّحِيْمِ

Imam Zainul Abidin (a.s.) na Malezi kwa Njia ya Dua

Mwenyezi Mungu (azza wa jalla) amewaamrisha waja wake kumuomba dua na kuomba haja mbalimbali kutoka kwake katika Aya nyingi ndani ya Qur'an tukufu, katika kitabu chake kitukufu anasema:

وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ

"Na Mola Wenu amesema: Niombeni nitawaitikia." [2]

Na amesema (Azza wa jalla):

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ.

"Na waja Wangu watakapokuuliza habari Yangu, Mimi niko karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi nawaniitikie Mimi na waniamini Mimi ili wapate kuongoka". [3]

Hakika Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) amechukua dhamana ya kumjibu yule anayemuomba kwa ikhlas na yakini, na kuanzia hapa ni juu ya mwanadamu muumini wakati wa kuomba haja yake amwelekee Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) kwa kumuomba dua ili amkidhie haja zake za duniani na akhera.

Na kuhusu fadhila za dua na utukufu wake, zimepokewa riwaya chungu nzima bali mutawatiri, zote zinatilia mkazo juu ya utukufu na fadhila za dua, na athari yake chanya katika kukidhi haja mbalimbali, na kufanikisha malengo ya duniani na akhera.

Hakika imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) amesema:

---

2. Surat al-Mu'min (al-Ghafir): 40:60
3. Surat al-Baqarah: 2:186.

الدُّعاءُمُخُّ العِبَادةِ

"Dua ni ubongo wa ibada". [4]

Na amesema (s.a.w.w.):

الدُّعاءُسِلاَحُ المُؤْمِنِ وَعَمودُ الدِّينِ وَنُورُ السَّمَاواتِ والأَرْضِ.

"Dua ni silaha ya muumini, nguzo ya dini na nuru ya mbinguni na ardhini".[5]

Pia (s.a.w.w). amesema:

مَا مِنْ شَيءٍ أَكرَمَ عَلَى اللهَ تَعَالَى مِنَ الدُّعَاءِ.

"Hakuna kitu kilicho bora zaidi kwa Mwenyezi Mungu kama vile dua".[6]

Na imepokewa kutoka kwa Mtume (s.a.w.w) amesema:

"Watu wawili wataingia peponi ambapo walikuwa wakitenda amali moja (hapa duniani) basi mmoja wao atamuona mwenzake yuko juu yake kidaraja, hapo atasema: Ewe Mola wangu mlezi! Kwa kitu gani umempa yeye na hali ya kuwa amali yetu ni moja Mwenyezi Mungu atasema: Ameniomba na wewe hukuniomba".

Kisha akasema:

سَلُوا (اسألوا) اللهَّ وأجزِلُوا، فإنَّهُ لا يَتَعَاظَمُهُ شيءٌ

"Muombeni Mwenyezi Mungu na zidisheni maombi, kwani yeye hakuna kitu kingine hukiona adhimu kama maombi".[7]

Na imepokewa kutoka kwa Amirul-Muuminina Ali (a.s.) :amesema:

---

4. Mustadrak al-Wasaeel, al-Tabrasi, Juz. 5, uk. 167, Namba: 5576.
5. Usul al-Kaafiy, al-Sheikh kulayni, Juz. 2, uk. 439, Namba: 1.
6. Bihar al-Anwaar, al-Allama Majlisi, Juz 90, uk. 294,
7. Bihar al-Anwar, Juz. 90, uk. 302, Na Wasail al-Shia, al-Hur al-Amili, Juz. 7, uk. 24, Namba: 8605.

أَحَبُّ الأعمالِ إلى اللهِ عزَّ وجلّ فِي الأرضِ الدُّعَاءُ

"Amali inayompendeza zaidi Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) ardhini ni dua".[8]

Na Imam Sadiq (a.s.) amesema:

عَلَيكَ بِالدُّعَاءِ، فإنَّ فيهِ شِفاءً مِنْ كُلِّ داءٍ

"Ni juu yako kuomba dua, hakika ndani yake kuna ponyo la kila ugonjwa".[9]

Na hakika amepokea Muawiya bin Ammar amesema:
Nilimwambia Abu Abdillah (a.s.):

جعلني الله فداك، ما تقول في رجلين دخلا المسجد جميعاً، كانَ أحدهما أكثر صلاة، والآخر دعاء، فأيهما أفضل؟

Nimejitoa kwa Mwenyezi Mungu fidia kwako, unasemaje kuhusiana na watu wawili walioingia msikitini pamoja, mmoja wao akaswali sana na mwingine akaomba dua sana, basi yupi kati yao ni bora zaidi Akasema: Wote wamefanya vizuri. Nikasema: Hakika nimejua, lakini ni yupi kati yao ni mbora zaidi?

Akasema: Yule aliyezidisha kufanya maombi, je, hujui kauli ya Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) isemayo:

ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ.

Niombeni nitakujibuni? [10]

Mpaka mwisho wa Aya. [11]

Hadithi hizo na nyinginezo zinatilia mkazo juu ya fadhila ya dua, na kwamba hiyo ni katika aina za ibada, na kwa hiyo ni muhimu

8. Wasail al-Shia, al-Hur al-Amili, Juz. 7, uk. 31, Namba: 8628.
9. Usul al-Kaafiy, al-Sheikh al-Kulayni, Juz. 2, uk. 470, Namba: 1.
10. Surat al-Mu'min (al-Ghafir): 40:60.
11. Majmu' al-Bayaan fi Tafsirul Qur'an, al-Allama al-Tabrasi, Juz. 8, uk. 823.

na kuna fadhila kubwa zinazopatikana kwa usomaji wa dua zilizopokewa kutoka kwenye ndimi za Maimamu (a . s.) na pia kufahamu maana yake, madhumuni yake na mafuhumu zake, aidha kubobea katika dalili zake kiroho, kimalezi na kitabia.

SAHIFAT SAJJADIYA NA MALEZI KWA NJIA YA DUA

Imam Ali bin Husein Zainul Abidin (a . s.) ameupatia umma wa kiislamu hazina ya maarifa ya kina ya kiislamu na madhumuni muhimu katika itikadi, fikra, tabia, malezi na mwenendo.

Na hakika Imam Zainul Abidin (a. s.) ametumia dua kama njia ya malezi, kwa hakika ameweza kulea vizazi vya wanazuoni, wasomi, wapokezi wa hadithi na wafasiri kuhusiana na fadhila za tabia na mwenendo wake. Ni kituo chake cha malezi ambapo alitumia njia ya dua, na hakika wamehitimu katika chuo chake cha elimu mabingwa katika elimu na maarifa, viongozi wa watoa rai na fikra na kufikia kilele cha juu katika elimu mbalimbali na maarifa ya kiislamu.

Na kitabu Sahifat Sajjadiya ambacho kina dua muhimu mno hakikujikita tu katika maombi, dua na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu aliyetukuka, bali hakika pia kina hazina ya elimu na maarifa ya kutosha ya kiislamu kutokana na yale yaliyomo katika maswala mbalimbali kama vile masuala ya kiitikadi, kijamii, kitabia, malezi n.k.

Na miongoni mwa yale yanayojulisha umuhimu na thamani kilichonacho kitabu Sahifat Sajjadiya makumi ya vitabu fafanuzi v i m e a n d i k w a, na mhakiki mkubwa Agha Buzurghi Tehrani, amekusanya vitabu fafanuzi 150 katika kitabu chake chenye thamani na hadhi kubwa kinachoitwa Adhariatu Ila Taswanif S h i a h. Aidha kitabu hiki Sahifat Sajjadiya kimefanyiwa tarjuma katika lugha mbalimbali za ulimwenguni.

Na kitabu Sahifat Sajjadiya kina maana na dalili za malezi yaliyo

m u h i m u, pia zipo ishara mbalimbali za kitabia, mwenendo na kiroho ili kumlea mwanadamu katika fadhila za kinafsi na ukamilifu wa kiroho.

Na kutokana na dua tukufu za Imam Zainul Abidin (a.s.) ambazo alizisambaza kwa watu aliweza kulea kundi kubwa la waumini na kukabiliana na ufisadi na uovu ambao ulianza kuenea sehemu kubwa katika nyanja zote za maisha kwa kutumia dua.

Hakika umuhimu ulionao kitabu Sahifat Sajjadiya ndiyo maana kikapewa jina la Injili ya Ahlul-Bayt na Zaburi ya Aali M u h a m m a d. Aidha huhesabiwa ni kitabu kilichokusanya fani mbalimbali za kiarabu na ufasaha na kinafuatia kiubora baada ya kitabu Nahjul–Balagha kutokana na thamani na ufasaha wa hali ya juu, kwa umuhimu wake mkubwa hakika Marjaa Ayatullah Udhma Mar'ashi Najafi aliyefariki mwaka 1353 Hijiria, alimtumia nakala ya kitabu Sahifat Sajjadiya Allamah wa zama hizi mwandishi wa Tafsiri Sheikh Twantwawi Mufti wa Iskandariya, basi baada ya kumshukuru yeye kutokana na zawadi hiyo akaandika hivi:

ولسوء حظنا هو اننا لم نحصل على هذا العمل القيم والخالد الذي هو تراث النبوة، وكنت كلما أنظر فيها أراها فوق كلام المخلوق و دون كلام الخالق.

"Na hadhi yetu mbaya, na sisi hatukuwa wenye kuipata amali hii yenye thamani na ya kudumu, nayo ni urithi wa utume, na kila pale ambapo nilikuwa ninaangalia ndani yake nimeona kipo juu ya maneno ya kiumbe na chini ya maneno ya muumba".[12]

Na Sahifat Sajjadiya Al-Kamilah kina dua zaidi ya 70, nazo ni:

1. Dua yake katika kumhimidi na kumsifu Mwenyezi Mungu Mtukufu.
2. Dua yake katika kumtakia Rehema Mjumbe wa

12. Seeratul Aimma al-Ithnaashar, Mahdi al-Bishwaee, uk. 241.

Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).
3. Dua yake kwa ajili ya Malaika wabebao Arshi, na kwa kila Malaika aliyewekwa karibu.
4. Dua yake katika kuwatakia Rehema wafuwasi wa Mitume.
5. Dua yake kwa ajili yake mwenyewe, na kwa ajili ya walio chini ya mamlaka yake.
6. Dua yake katika nyakati za Asubuhi na Jioni.
7. Dua yake anapotokewa na jambo muhimu au kufikwa na taabu na tatizo.
8. Dua yake katika kujilinda na mambo yachukizayo, tabia mbaya na matendo yalaumiwayo.
9. Dua yake wakati akiwa na shauku sana ya kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
10. Dua yake aombapo kimbilio kwa Mwenyezi Mungu.
11. Dua yake kwa ajili ya hatima njema.
12. Dua yake katika kukiri na kuomba toba kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
13. Dua yake katika kumwomba haja Mwenyezi Mungu Mtukufu.
14. Dua yake endapo akifanyiwa uadui na aonapo asiyoyapenda toka kwa madhalimu.
15. Dua yake akiwa mgonjwa au akisumbuliwa na jambo au kupatwa na balaa.
16. Dua yake aombapo kujitoa kwenye dhambi zake au akinyenyekea kuomba msamaha kutokana na dosari zake.
17. Dua yake atajwapo Shetani hujilinda naye na hujilinda na uadui wake na vitimbi vyake.
18. Dua yake akiepushwa na jambo analolikhofia au kuharakishiwa ayatakayo.
19. Dua yake wakati wa kuomba mvua kipindi cha ukame.
20. Dua yake katika kuomba tabia njema na vitendo vya kumridhisha Mwenyezi Mungu.
21. Dua yake anapohuzunishwa na jambo au makosa kumhamanisha.
22. Dua yake katika shida, juhudi na mambo yanapokuwa magumu kwake.

23. Dua yake amwombapo Mwenyezi Mungu afya njema na anapoitolea shukurani.
24. Dua yake kwa ajili ya wazee wake (a.s.).
25. Dua yake kwa ajili ya watoto wake.
26. Dua yake kwa ajili ya majirani zake na marafiki zake.
27. Dua yake kwa watu wa mipakani.
28. Dua yake anapokimbilia kwa Mwenyezi Mungu.
29. Dua yake iwapo riziki yake imebana.
30. Dua yake kwa ajili ya kuomba msaada wa kulipa deni.
31. Dua yake kuidhikiri toba na kuiomba.
32. Dua yake baada ya kumaliza Swala za Usiku.
33. Dua yake katika kufanya Istakhara (kuomba Kheri Zaidi).
34. Dua yake apatwapo na balaa au amwonapo mwenye kupatwa na fedheha kwa ajili ya dhambi.
35. Dua yake katika hali ya ridhaa awaangaliapo wana wa dunia hii.
36. Dua yake aangaliapo mawingu na umulikaji, na asikiapo sauti ya radi.
37. Dua yake anapokiri upungufu wake katika kutekeleza shukurani ipasavyo.
38. Dua yake katika kuomba radhi ya matendo mabaya ya waja na kwa kutowajibika ipasavyo kukhusu haki zao, na katika kuikomboa shingo yake dhidi ya moto.
39. Dua yake katika kuomba msamaha na rehema.
40. Dua yake atangaziwapo kifo cha mtu au akumbukapo mauti.
41. Dua yake katika kuomba sitara na ulinzi.
42. Dua yake wakati wa kukhitimisha Qur'an.
43. Dua yake auonapo Mwezi Mwandamo.
44. Dua yake uingiapo Mfungo wa Ramadhani.
45. Dua yake katika kuuaga Mwezi wa Ramadhani.
46. Dua yake Siku Ya Idil-Fitri (Idi Ndogo) Na Ijumaa amalizapo kuswali baada ya kusimama na kuelekea Kibla.
47. Dua yake katika Siku ya Arafa.
48. Dua yake katika Siku Ya Idil-Adh'ha (Idi Kubwa) na siku ya Ijumaa.

49. Dua yake katika kujikinga na vitimbi vya maadui na kuzuia ubaya wao.
50. Dua yake katika hali ya woga.
51. Dua yake katika kusihi na kunyenyekea.
52. Dua yake katika kumsihi Mwenyezi Mungu Mtukufu.
53. Dua yake katika kujidhalilisha kwa Mwenyezi Mungu Mwenye Enzi na Utukufu.
54. Dua yake atakapo kuondoa mashaka.
55. Dua yake katika Tasbihi zake.
56. Dua yake katika Utukuzo wake.
57. Dua yake katika kuwataja Aali Muhammad (a.s.).
58. Dua yake katika kumsalia Adam (a.s.).
59. Dua yake awapo katika matatizo na atakapo kuomba faraja.
60. Dua yake dhidi ya yale anayojitahadharisha nayo na kuyaogopa.
61. Dua yake katika kujidhalilisha.
62. Dua yake Siku ya Jumapili.
63. Dua yake Siku ya Jumatatu.
64. Dua yake Siku ya Jumanne.
65. Dua yake Siku ya Jumatano.
66. Dua yake Siku ya Alkhamisi.
67. Dua yake Siku ya Ijumaa.
68. Dua yake Siku ya Jumamosi.
69. Dua 15 za maombi. [13]

Hivyo ndivyo Imam Zainul Abidin (a . s.) alivyokuwa akieleza kutokana na mtazamo wake kuhusu suala la malezi, tabia itikadi na utamaduni kupitia dua tukufu ambazo alikuwa akizisoma usiku na mchana, nazo zinabeba utaratibu kamili wa malezi ya mwanadamu kifikra, kimawazo, kimwenendo na kimfumo.

Na lengo la msingi na la muhimu ni kufikiria na kutafakari kuhusiana na dua zilizomo katika Sahifat Sajjadiya na kutotosheka kwa kuzisoma tu, bali kujituma katika kufahamu yale yaliyomo ndani ya dua hizo kuhusiana na mafuhumu, madhumuni, dalili mbalimbali za kina.

13. Rejea al-Sahifatu al-Sajjadiyya al-Kaamila

Na huhesabiwa malezi kwa njia ya dua ni miongoni mwa njia za kuitakasa nafsi, na kuisafisha roho, pia kukuza nguvu za kiroho na kiimani katika utu wa mwislamu. Na kulingana na umuhimu wa dua katika kumjenga mtu kiroho, hapa tutaeleza mambo muhimu katika malezi kwa njia ya dua na athari pia faida za dua. Kisha masharti ya kukubaliwa dua, na baada ya hapo tutaeleza vizuizi vya kukubaliwa maombi, na tutahitimisha maudhui hii kwa kuzungumzia baadhi ya dua zenye kujibiwa.

ATHARI ZA DUA

Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) amehimiza suala la dua, basi Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) katika kitabu chake anasema:

ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ.

"Niombeni nitawaitikia"[14]

Na akachukua dhamana kwa yule atakayemuomba bila shaka atamkubalia maombi yake, kwa hivyo ni wajibu kwa muumini anapokuwa na haja amwelekee Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) kwa kumuomba dua, ili akidhiwe haja zake za duniani na akhera.

Na siyo jambo la uficho kwamba dua ina athari chanya na faida chungu tele, hapa tutazielezea zilizo muhimu zaidi katika dondoo zifuatazo:

1. Hakika dua ni kiunganishi baina ya mwanadamu na muumba wake, kwa hali hiyo mja anamuomba Mungu wake mlezi akitaka kwake msamaha na usamehevu kutokana na makosa yake, kuteleza kwake na madhambi yake. Na Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) ni mwenye huruma zaidi kwa waja wake, basi dua ni mlango miongoni mwa milango ya rehema za Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) kwa waja wake.

2. Hakika dua hukuza nguvu ya kiroho kwa mwanadamu, kwa hivyo dua ina athari kubwa katika kukuza upande wa

14. Surat al-Mu'min (al-Ghafir): 40:60.

kiroho na kimaanawi, hasa hasa pale mwanadamu anapodumisha usomaji wa dua zilizopokewa kutoka kwa Maimamu wa Ahlul- B a y t (a . s .) kwa maana ambayo zinahusiana na kujidhalilisha, kuwa na khofu, unyenyekevu na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla).

3. Mwanadamu anaweza kufanikisha haja zake za duniani na akhera kupitia dua, Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) anasema:

ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ.

"Na Mola Wenu amesema: Niombeni nitawaitikia".[15]

Na akasema:

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِي عَنِّي فَإِنِّي قَرِيبٌ أُجِيبُ دَعْوَةَ الدَّاعِ إِذَا دَعَانِ فَلْيَسْتَجِيبُوا لِي وَلْيُؤْمِنُوا بِي لَعَلَّهُمْ يَرْشُدُونَ.

"Na waja Wangu watakapokuuliza habari Yangu, Mimi niko k a r i b u . Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba. B a s i nawaniitikie Mimi na waniamini Mimi ili wapate kuongoka ".[16]

4. Dua inasaidia katika kuitakasa nafsi na kuutoharisha moyo, na kuusafisha ulimi, na huleta ladha ya uonjaji, usalama wa utamkaji na adabu nzuri katika kuzungumza na Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla).

5. Hakika dua zilizopokewa kutoka kwenye ndimi za Ahlul-bayti (a.s.) hubeba mafuhumu ya kina na madhumuni muhimu katika itikadi, tabia na malezi. Na hakika kudumisha usomaji wake huimarisha mafuhumu hayo katika utu wa muumini.

6. Hakika dua ni utaratibu wa kivitendo na kimwenendo katika kuitakasa nafsi, na kuinasua na tabia mbaya, na kukuza mambo mazuri ya fadhila na kujipamba na tabia njema.

MASHARTI YA KUKUBALIWA DUA

Ili dua iweze kukubaliwa na athari zake zipatikane na faida zake

15. Surat al-Mu'min (al-Ghafir): 40:60.
16. Surat al-Baqarah: 2:186.

pia, inapaswa kushikamana na masharti na adabu za dua, na zile zilizo muhimu zaidi ni:

1. Kumjua Mwenyezi Mungu (azza wa jalla) Kumuomba Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) ni chimbuko la maarifa au kumjua yule unayemuomba, wala dua zetu zisiwe ambazo hazimjui Yeye (Azza wa Jalla), hakika imepokewa kutoka kwa Imam Kadhim (a.s) amesema: "Watu walimwambia Imam as-Sadiq (a.s.) Tunaomba hatujibiwi! Akasema:

لَاتَكُمْ تَدْعُوْنَ مَنْ لَّا تَعْرِفُوْنَهُ

"Hakika nyinyi mnamuomba msiyemjua." 17

Basi yule anayemuomba Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) akiwa na elimu, maarifa na itikadi sahihi inatofautiana na yule ambaye anamuomba Mwenyezi Mungu hali ya kuwa hamjui kwa uhakika wake.

2. Kutekeleza Maamrisho ya Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla): Miongoni mwa masharti ya kujibiwa dua ni kutekeleza kivitendo maamrisho ya Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla), ikiwa ni pamoja na kujiepusha na yale aliyoyakataza. Hivyo kutekeleza mambo ya wajibu na kuacha mambo ya haramu ni sharti katika kujibiwa dua. Ama yule anayetenda mambo ya haramu, na yule anayetenda yale aliyoyakataza Mwenyezi Mungu na kujiingiza katika maasi wala hafanyi mambo ya wajibu haitojibiwa dua yake. Hivyo imepokewa kutoka kwa Imam Ali (a.s.) amesema:

الدَّاعي بلا عَمَلٍ كالرّامِي بِلَا وَتَرٍ

"Muombaji bila ya kujishughulisha ni kama vile mrushaji mshale bila kulenga shabaha".[18]

3. Kuhudhurisha Moyo: Kuelekeza moyo, viungo na hisia wakati wa kuomba kwa yule tumuombaye ambaye sio mwingine bali ni Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla), basi

17. Bihar al-Anwar, al-Allama al-Majlisi, Juz. 90, uk. 368, Hadith 4,

18. Nahjul Balagha: Juz. 4, uk. 740, Namba: 338. al-Khisal, al-Sheikh al-Saduq, uk. 621.

kuhudhurisha moyo ni sharti katika kujibiwa dua, ama yule mwenye moyo wenye kughafilika basi hatajibiwa dua yake. Mtume (s.a.w.w.) amesema:

لا يَقبَلُ اللهَ دُعَاءَ قَلبٍ ساهٍ

"Mwenyezi Mungu haikubali dua ya moyo ulioghafilika".[19]

Pia imepokewa kutoka kwake (s.a.w.w.) amesema:

اغتَنِموا الدُّعَاءَ عند الرِّقَّةِ فإنَّها رحمةٌ

"Faidikeni na dua wakati wa mlainiko wa moyo, kwani hiyo ni rehema".[20]

Na Imam Ali (a.s.) amesema:

لا يَقبَلُ اللهَ دُعَاءَ قَلبٍ لاهٍ

"Mwenyezi Mungu haikubali dua ya moyo wa mpuuzi".[21]

Na Imam as-Sadiq (a.s.) amesema:

إنَّ اللهَ عزّوجلّ لا يَستَجِيبُ دُعَاءً بِظَهرِ قلبٍ ساهٍ، فإذا دَعَوتَ فَأقبِلْ بقلبِكَ، ثمّ استَيقِنْ بالإجابَةِ.

"Hakika Mwenyezi Mungu aliyetukuka haikubali dua kwa dhahiri ya moyo wa aliyejisahau, na utakapoomba basi uelekee kwa moyo wako, kisha uwe na yakini na majibu".[22]

Aidha imepokewa kutoka kwake (a.s.) amesema:

إذا اقشَعَرَّ جِلدُكَ و دَمَعَتْ عَيناكَ ووَجِلَ قلبُكَ فَدُونَكَ دُونَكَ فقد قُصِدَ قَصدُكَ.

---

19. Wasail al-Shia, al-Hur al-Amili, Juz. 7, uk. 53, Namba: 8701.
20. Bihar al-Anwar, Juz. 90, uk. 313.
21. Bihar al-Anwar, Juz, 90, uk. 314, Hadith 19.
22. Usul al-Kaafiy, Juz. 2, uk. 444, Hadith 1.

"Pindi ngozi yako ikisisimka na macho yako yakatoa machozi na moyo wako ukawa na khofu, basi lengo lako litafikiwa".[23]

Basi hata pale dua yetu inapojibiwa ni juu yetu kuamiliana na dua wakati wa kuisoma kimakini na kimazingatio, na iwe kwa hisia zetu, hakika sisi tunamzungumzisha Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla).

4. Chumo la Halali: Kazi ya heshima, na kutafuta riziki ya halali na kuhudumia familia ni miongoni mwa amali bora zaidi, na pale ambapo mtu ajitafutiapo riziki ya halali, na matendo ya halali, kwa hakika hilo husababisha au huacha athari chanya moyoni na akilini, na hupelekea kujibiwa dua. Mtume (s.a.w.w.) amesema:

من أحبّ أن يستجاب دعاؤه فليطيّب مطعمه ومكسبه.

"Yule anayetaka dua yake ikubaliwe basi kiwe cha halali chakula chake na chumo lake."[24]

Na Imam as-Sadiq (a.s.) amesema:

إذا أرادَأحدُكُم أن يُستَجَابَ لَهُ فَليُطَيِّبْ كَسبَهُ و لْيَخرُجْ مِن مَظَالِمِ الناسِ، وإنَّ اللهَ لا يُرفَعُ إلَيهِ دُعاءُ عبدٍ وفي بَطنِهِ حرامٌ أو عندَهُ مَظلِمَةٌ لِأَحَدٍ مِن خَلقِهِ.

"Mmoja wenu akitaka dua yake ikubaliwe basi chumo lake liwe la halali na aache kuwadhulumu watu. Na hakika Mwenyezi Mungu haipokei dua ya mja hali ya kuwa tumboni mwake kuna haramu au amemdhulumu yeyote miongoni mwa viumbe wake".[25]

5. Moyo Mkunjufu: Miongoni mwa adabu za dua na masharti ya kujibiwa dua ni iwe yenye ikhlas, Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) anasema:

---

23. Usul al-kaafiy, al-Sheikh al-kulayni, Juz. 2, uk. 478, Namba: 8.
24. Bihar al-Anwar, Juz. 90, uk. 372.
25. Bihar al-Anwar, Juz, 90, uk. 321, Hadith 31.

هُوَ الْحَيُّ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَادْعُوهُ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ

"Yeye yuko hai – hapana mungu isipokuwa Yeye. B a s i mwabuduni Yeye mkimsafia Dini Yeye. Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote".[26]

Na dua iwe ya unyenyekevu na katika uficho kama Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) anavyosema:

ادْعُوا رَبَّكُمْ تَضَرُّعاً وَخُفْيَةً

"Mwombeni Mola Wenu kwa unyenyekevu na kwa uficho. Hakika Yeye hawapendi wapetukao mipaka".[27]

Na dua iwe inatokana na khofu na kutumai kama ilivyo katika kauli yake (Azza wa Jalla).

وَادْعُوهُ خَوْفاً وَطَمَعًا

"na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai".[28]

Nyakati Tukufu :

Dua ni jambo linalotakiwa katika kila wakati na zama, lakini zipo baadhi ya nyakati hujibiwa dua zaidi pia hutiliwa mkazo wa kujibiwa dua kama vile siku ya Ijumaa, siku ya Arafa, usiku wa cheo Laylatul-Qadri, wakati wa kunyesha mvua, wakati wa k u s w a l i, wakati wa mkesha, na wakati wa mawio mawili. Amirul–Muuminina (a.s.) amesema:

اغْتَنِموا الدُّعَاءَ عِنْدَ أَرْبَعٍ: عِنْدَ قِرَاءَةِ الْقُرْآنِ، وَعِنْدَ الأَذَانِ، وَعِنْدَ نُزُولِ الْغَيْثِ، وعِنْدَ الْتِقَاءِ الصَّفَّيْنِ لِلشَّهَادَةِ.

"Nufaikeni na dua katika mambo manne wakati wa kusoma Qur 'a n i, wakati wa adhana, wakati wa kunyesha mvua, na mistari

26. Surat al-Mu'min (al-Ghafir): 40:65.
27. Surat al-A'araf: 7:55.
28. Surat al-A'araf: 7:56.

miwili inapokutana kwa ajili ya kutoa shahada (jihadi)".[29]

Na imepokewa kutoka kwa Sakuni, kutoka kwa Ja'far bin Muhammad, kutoka kwa baba yake (a.s.) amesema:

اغتنموا الدعاء عند خمس: عند قراءة القرآن، وعندالأذان، وعند نزول الغيث، وعند التقاء الصفين للشهادة، وعند دعوة المظلوم ليس لها حجاب دون العرش.

"Faidikeni na dua katika sehemu tano wakati wa usomaji wa Qur'ani, wakati wa adhana, wakati mvua inanyesha, inapokutana mistari miwili kwa ajili ya kutoa shahada (jihadi) na dua ya mdhulumiwa haina kizuizi chini ya Arshi".[30]

VIZUIZI VYA KUJIBIWA DUA

Vipo vizuizi vinavyozuia dua kujibiwa, na vilivyo muhimu zaidi ni:

1. Kutenda Mambo ya Haramu na Yaangamizayo:

Hakika binadamu anapotenda mambo ya haramu yenye kuangamiza na maasi, na kuendelea kuyatenda na kutotubia, kwa hakika hayo huwa ni kizuizi cha kukubaliwa kwa dua. Amirul–Muuminina Ali (a.s.) amesema:

لا تَستَبطِئْ إجابَةَ دُعَائِكَ وقد سَدَدتَ طريقَهُ بِالذُّنوبِ.

"Usicheleweshe dua yako kujibiwa na hakika umezuia njia kwa kutenda madhambi".[31]

2. Kudhulumu Waja:

Kuwatendea dhuluma waja wa Mwenyezi Mungu, au ubaya dhidi

29. Usul al-kaafiy, al-Sheikh al-Kulayni, Juz. 2, uk. 477, Namba: 3.
30. Al-Amaali, al-Sheikh al-Suduq, uk. 327, Namba: 393, Wasaail al-Shia, al-Hur al-Amili, Juz. 7, uk. 65, Namba: 8739.
31. Uyun al-Hikam wal-Mawaaeedha, uk. 524, Mizanul Hikma, Muhammad Ray Shahri, Juz. 3, uk. 884.

ya wengine, au dhidi ya jamaa zako na familia yako kama vile m k e o, watoto wako, wazazi wako, ndugu zako wa karibu, hilo hupelekea kuzuiwa dua. Imam Ali (a.s.) amesema:

مَن عَذَرَ ظالماً بظُلمِهِ سَلَّطَ اللهَ علَيهِ مَن يَظلِمُهُ فإنْ دعا لَم يُستَجَبْ لَهُ، ولَم يَأجُرْهُ اللهَ على ظُلامَتِهِ.

"Yule ambaye humsamehe dhalimu kwa dhuluma zake, Mwenyezi Mungu atammakinisha juu yake yule a t a k a y e m d h u l u m u, na ikiwa ataomba dua haitojibiwa, na Mwenyezi Mungu hatomlipa malipo kwa kudhulumiwa kwake". [32]

3. Kutoamrisha Mema na Kukataza Maovu:

Hakika kutotekeleza majukumu ya kijamii, kuwaelekea waovu na w a p o t o k a j i, na wale ambao wanatenda maovu, na wanaozuia m e m a, ni miongoni mwa sababu za kutokubalika dua. Na kama vile dua inakuwa katika mambo ya mtu binafsi, pia inakuwa katika mambo ya kijamii, na pindi jamii itapopatwa na tatizo au janga au msiba basi ni juu yake kumuomba Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) mpaka Mwenyezi Mungu awaondolee hilo lililowafika miongoni mwa mabalaa, mitihani na machukizo. Lakini ikiwa jamii haitekelezi jukumu la kuamrisha mema na kukataza mauvu, vyovyote watakavyomuomba Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) hatojibu maombi yao kwa yale waliyoyaacha kuhusiana na faradhi hizi za kiislamu. Mtume (s.a.w.w.) amesema:

لتأمُرُنّ بالمعروفِ و لَتَنهُنَّ عَنِ المُنكَرِ، أو لَيُسلِّطَنَّ اللهَ شِرارَكُم علَى خِيارِكُم، فيَدعو خِيارُكُم فلا يُستجابُ لَهُم.

"Amrisheni mema na katazeni maovu au Mwenyezi Mungu awamakinishe waovu wenu juu ya wema wenu, basi watu wema wataomba wala hawatojibiwa".[33]

---

32. Wasail al-Shia, al-Hur al-Amili, Juz. 16, uk. 56, Namba:20966.
33. Bihar al-Anwar, al-Allama al-Majlisi, Juz. 90, uk. 378, Namba:21.

4. Kula Vitu vya Haramu:

Ikiwa chumo la mtu linatokana na haramu, na amali yake ya haramu kama vile kufanya biashara ya mihadarati, au kujitwalia mali za watu kwa njia ya wizi na uporaji, au kula mali za watu kwa batili, basi huyu ni miongoni mwa wale wasiojibiwa maombi yao. Imepokewa kwamba Nabii Musa (a.s.) alimuona mtu mmoja akinyenyekea unyenyekeaji mkubwa na akiomba hali ya kuwa mikono yake ameinua juu, basi Mwenyezi Mungu akamfunulia Nabii Musa (a.s.).

رأى رَجُلًا يَتَضرَّعُ تَضَرُّعاً عظيماً، ويَدعو رافعاً يَديهِ و يَبتَهِلُ، فَأوحَى اللهَ إلى موسى (ع): لو فَعَلَ كذا و كذا لَما اسْتُجيبَ دُعاؤهُ، لأنَّ في بطنِهِ حراماً، وعلى ظَهرِهِ حراماً، وفي بيتِهِ حراماً.

"Lau angelifanya hivi na vile nisingelimkubalia maombi yake, kwani tumboni mwake kuna haramu, na nyumba yake ni ya haramu." Basi kula mali ya haramu, na kuishi kwa kutumia vitu vya haramu, kuuza vyakula na vinywaji vinavyotokana na haramu huuchafua moyo na kuufanya mweusi, na kwa hivyo hatakubaliwa yeye dua yake.[34]

5. Maslahi ya Mja:

Huenda muumini asijibiwe dua yake, au ikacheleweshwa miaka kadhaa kwa maslahi ya mja mwenyewe, basi Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) ni mjuzi kwa yale yenye maslahi kwa kiumbe, hivyo huenda hekima ya kiungu ikalazimu kutojibu maombi wakati hakuna kizuizi chochote kati ya vizuizi vilivyotangulia, na hakika maslahi ndiyo hupelekea hivyo. Imepokewa kutoka kwa Is'haq bin Ammar amesema: Nilisema kumwambia Abu Abdillah (a.s.):

يُستَجَابُ للرجلِ الدُّعاءُ ثمّ يُؤَخِّرُ؟ قال (ع): نَعَم عِشرونَ سَنةً.

---

34. Mahaj ad-Duwaat: uk. 24, Hadith 34, Bihar al-Anwar, al-Allama al-Majlisi, Juz. 90, uk. 372, Namba: 14.

"Mtu hukubaliwa dua yake kisha hucheleweshewa Akasema: Ndiyo, hata miaka ishirini".[35]

AINA ZA DUA ZENYE KUJIBIWA

Zipo nyingi lakini zilizo muhimu mno, ni hizi zifuatazo:

1. Dua ya Mzazi kwa Mwanawe: Pale Anapomtendea Wema au Ubaya:

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) amesema:

ثلاثُ دَعَواتٍ لا يُحجَبنَ عن اللهَ تَعالى: دعاءُ الوالِدِ لولدِهِ إذا بَرَّهُ، ودعوتُهُ عَلَيهِ إذا عَقَّهُ. ودعاءُ المظلومِ على ظالمِهِ، ودعاؤهُ لَمِن انتصَرَ لَهُ مِنْهُ.

"Dua aina tatu hazina kizuizi kwa Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) dua ya mzazi kwa mwanawe anapomtendea wema na ubaya, dua ya mdhulumiwa kwa aliyemdhulumu, na dua yake kwa yule aliyemnusuru."[36] Na katika wema wa mtu kwa wazazi wawili na kuwatendea wema hao wawili, ni kuwaombea hao wawili, basi usiwasahau kuwaombea dua hasa hasa katika nyakati tukufu zilizotiliwa mkazo kama vile siku ya Ijumaa, siku ya Arafa, usiku wa cheo, usiku wa manane. Na dua zilizo nzuri zaidi katika upande huu na bora zaidi ni dua ya Imam Sajjad (a.s.) kwa wazazi wake wawili, basi tudumishe kuisoma!

2. Dua ya Mdhulumiwa kwa Aliyemdhulumu:

Imepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuhusiana na dua ya mdhulumiwa kuwa ni yenye kujibiwa, pale aliposema:

اتقوا دعوة المظلوم، فإنما يسأل الله تعالى حقه، وإن الله تعالى لم يمنع ذا حق حقه.

35. Bihar al-Anwar, al-Allama al-Majlisi, Juz. 90, uk. 375, Namba: 16.
36. Wasail al-Shia, al-Hur al-Amili, Juz. 7, uk. 130, Namba: 8921.

" Iogopeni dua ya mdhulumiwa kwani anapoomba hakika Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) hamzuii mwenye haki kupata haki yake."[37] Na amesema (s.a.w.w.):

اتقوا دعوة المظلوم، فإنها تصعد إلى السماء كأنها شرارة.

"Iogopeni dua ya mdhulumiwa hakika hiyo hupanda mbinguni kama vile cheche za moto."[38] Na pindi Imam Ali (a.s.) alipoulizwa: Ni masafa gani yaliyopo kati ya ardhi na mbingu Akasema:

بين السماء والأرض مد البصر، ودعوة المظلوم.

"Baina ya mbingu na ardhi ni upeo wa macho, na dua ya mdhulumiwa".[39]

3. Dua ya Muumini kwa Muumini:

Miongoni mwa dua zenye kujibiwa ni dua ya muumini kwa muumini mwenzake hasa hasa asipokuwepo, na huenda akawa muumini mwenzake ni mwenye Ikhlas na yakini basi hukubaliwa dua yake. Hakika imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) amesema:

دعاء المؤمن للمؤمن يَدفَعُ عنهُ البلاءَ ويُدِرُّ عَليهِ الرزقَ.

"Dua ya muumini kwa muumini mwenzake humuondolea yeye mabalaa na huongeza riziki".[40]

---

37. Kanzul Ummal, Juz. 3, uk. 499, Hadith. 7597, Mizanul Hikma, Muhammad Rayb Shahri, Taasisi ya Darul Hadith, Beirut- Lebnan, Chapa ya pili 1419 Hijiria, Juz. 4, uk. 1781, Namba: 11491.

38. Kanzul Ummal, Juz. 3, uk. 499, Hadith. 7601, Mizanul Hikma, Muhammad Ray Shahri, Taasisi ya Darul Hadith, Beirut-Lebnan, Chapa ya Pili 1419 Hijiria, Juz. 4, uk. 1781, Namba: 11495.

39. Bihar al-Anwar, Juz. 55, uk. 93, Hadith. 14, Mizanul Hikma, Muhammad Ray Shahri, Taasisi ya Darul hadith, Beirut-Lebnan, Chapa ya pili 1419 Hijiria, Juz. 4, uk. 1781, Namba: 11497.

40. Bihar al-Anwar, al-Allama al-Majlisi, Juz. 71, uk. 222, Namba: 2.

4. Dua ya Yule Anayesoma Qur'an na Anadumisha Kuisoma:

Miongoni mwa dua zenye kujibiwa ni dua ya yule anayesoma Qur'an na hudumisha kuisoma kila wakati, kila zama na mahali. Amirul-Muuminina (a.s.) amesema:

اغتنموا الدعاء عند أربع: عند قراءة القرآن....

"Faidikeni na dua katika mambo manne wakati wa kusoma Qur'ani...."[41] Na inampasa muumini awe na hamu kubwa ya kusoma dua zilizopokewa kutoka kwa Maimamu wa Ahlul–Bayt watakatifu kwa yale yaliyomo miongoni mwa mafuhumu na madhumuni ya kiitikadi, kiakhlaki, kitabia na kimaanawi. Dua hizi zina uwezo wa kuathiri katika moyo na roho ikiwa mtu atazisoma kwa hisia na kuhudhurisha moyo, kwani huacha athari chanya katika silka ya mtu na kitabia yake, na humkuza kiroho na kimaanawi kwa kuimarisha roho ya dini katika shakhsia ya mwislamu.

IMAM ZAINUL ABIDIN (A.S) NA UKOMBOZI WA WATUMWA

Mataifa mbalimbali yamejulikana tangu zamani kwa utumwa, nao ni mwanadamu kutaka kummiliki mwanadamu mwenzake, na hakika jambo hilo lilitekelezwa kabla ya Uislamu na baada yake, na mwanadamu hawakuondokana nalo kwa njia ya sheria rasmi za kimataifa isipokuwa katika karne ya 20 AD. Na hakika Uislamu umehamasisha sana suala la kuwaacha huru watumwa na kuwakomboa, na hilo ni kutokana na njia mbili muhimu za hekima, nazo ni:

Njia ya kwanza:

Kuhamasisha suala la kuwaacha huru watumwa na kuwakomboa, na kulizingatia hilo ni miongoni mwa mambo bora zaidi ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) kama pia ilivyofanywa suala la kumuacha huru mtumwa ni kafara za makosa mengi ya jinai ambayo mwislamu anayatenda makosa hayo

41. Usul al-kaafiy, al-Sheikh al-Kulayni, Juz. 2, uk. 477, Namba: 3.

huwajibika kumwacha huru mtumwa, kama vile kufungua katika mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa makusudi, kafara ya kuvunja yamini, kafara ya nadhiri na kafara ya kumuua mtu kwa makosa..... n.k.

Njia ya pili:

Kufunga njia zote zinazopelekea kuwepo utumwa, hakika Uislamu umefunga sababu nyingi na njia ambazo zinapelekea utumwa isipokuwa hali moja tu, nayo ni kuwafanya mateka wa vita watumwa endapo tu, maadui watawachukua Waislamu mateka na kuwafanya watumwa. Na hiyo ni kwasababu washirikina na makafiri walikuwa wakiwafanya watumwa mateka wa kiislamu. Hiyo ni kama inavyoruhusiwa kuamiliana na mateka kwa majigambo na fidia kama anavyosema katika kauli yake:

فَإِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّى إِذَا أَثْخَنتُمُوهُمْ فَشُدُّوا الْوَثَاقَ فَإِمَّا مَنًّا بَعْدُ وَإِمَّا فِدَاءً حَتَّى تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا

> "Basi mnapokutana na waliokufuru wapigeni shingo, mpaka mkiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vitue mizigo yake."[42]

Basi Uislamu ulikuwa ukihamasisha kuwaacha huru watumwa kwa upande mmoja na kwa upande mwingine ulikuwa ukizingatia kufanya biashara ya watu ni kati ya biashara inayochukiza zaidi na karaha zaidi.

Imam na Watumwa:

Kwa hakika suala la watumwa ni miongoni mwa masuala yaliyopatikana katika jamii ya watu na hasa hasa katika karne zilizopita ambapo suala hilo lilikuwa kati ya mambo yaliyoenea, na miongoni mwa desturi zilizokubalika katika jamii, kwa namna ambayo walitumia kuwatumikisha na kuwafanya watumishi wa majumbani, hususani katika majumba ya watukufu, waheshimiwa

42. Surat Muhammad: 47:4.

na mabwanyenye.

Na katika zama za Imam Zainul Abidin (a.s.) utumwa ulienea sana katika jamii, nao ulikuwa ni matokeo ya kuingia Waislamu katika miji mingine, na kupanuka wigo wa kijiografia, kwani Imam Zainul–Abidina (a.s.) aliishi katika zama za utawala wa Abdul-Malik bin Marwan na mwanawe Al-Walid bin Abdul-Malik. bin Marwan alielekea yeye mwenyewe Hijaz na Iraq baada ya kumalizika vuguvugu la Zubeiriya, na Uislamu ukaenea zaidi hasa hasa Afrika, na aliweza kupata ngawira kutokana na mali zisizohesabika miongoni mwa dhahabu na vito vinginevyo, ilikuwa ni mali nyingi mno mpaka wanahistoria wakawa na ibara isemayo:

ما الله أعلم به

"Ambayo Mwenyezi Mungu ndiye ajuaye zaidi wingi wake".[43]

Na katika Andalusia (Hispania) Tarik bin Ziyad na Musa bin Naswir waliweza kuipata meza ya chakula na kiti cha Nabii Suleiman (a.s.) na utajiri huu kwa hali ya kawaida uliinua hali ya maisha ya kijamii hususani ya watawala na wale wenye nafasi na madaraka katika jamii ya watu, ambapo wao walikuwa wakimpelekea mtawala zawadi mbalimbali na vitu vingine vingi na hukidhi haja zao achilia mbali vile vilivyothibiti kutolewa kila mwaka.

Vivyo hivyo Waislamu walipata ngawira kutoka katika miji hiyo zaidi ya mateka elfu sitini na wakabadilika hao na kuwa watumwa kwa kuingia katika umma,[44] na ipo ibara ya andiko la Ibn Athiri nayo ni hii: Basi wakafikia 60,000 miongoni mwa mateka na hakutaja yeyote kwamba amesikia idadi kubwa zaidi ya hiyo.[45]

Na pindi jeshi la kiislamu lilipokuwa likiishi Damascus Syria

43. Al-Kaamil fil Tarikh, Ibn al-Athir, Juz. 4, uk. 277, Tarikh al-Tabari, Juz. uk. 19.
44. Taasisi al-Ima Abideen, al-Sheikh Muhsin al-Huseini, juz. 2, uk. 122.
45. Al-Kaamil fil Tarikh, Ibn al-Athir, Juz. 4, uk. 252.

lilichukuwa vijakazi bikira 30,000 kama ilivyoelezwa na baadhi ya wanahistoria.

Na jambo hili lilipelekea kuwepo idadi kubwa ya wanamwari, vijakazi na watumwa majumbani katika jamii ya kiislamu, na hivyo kwa hakika zilipatikana athari za kijamii, kitamaduni, kitabia na malezi, nalo ni jambo ambalo lilikuwa linahitajia tiba muafaka na katika nyanja tofauti.

Na Imam Zainul Abidin (a . s.) aliamiliana na kundi hilo la watumwa muamala wa kibinadamu wa hali ya juu kabisa. Alifanya juhudi zake ili kuwainua kielimu, kidini na kitabia mpaka wengi wao wakabadilika na kuwa wadau na wafanya kazi na kuleta athari chanya katika jamii ya kiislamu.

وقد كانت ظاهرة الانجاب من الموالى غير مرغوب فيها من قبل أهل المدينة للوضع الاجتماعى أسبابه هو عدم الرغبة فى أن يكون الولد وفيه عرق غير عربى، وكانوا يرون أن ذلک يؤثر على موقع الابن بين الأمة فى كفائته أو احترام النا اليه، حتى كان موقع الامام زين العابدين (ع) فتغيرت نظرتهم لذلک۔

Kulikuwa na mtazamo duni katika kuwaelekea watumwa kwani lilikuwa ni jambo lisilopendwa na watu wa Madina kulingana na hali ya kijamii ambayo ilikuwa wakati huo, mtu kuzaa na mtumwa. Na miongoni mwa sababu kubwa zaidi ni kutokuwapo na utashi wa mtu kupata mtoto asiye mwarabu au kuona mwanawe haheshimiwi na watu, ilikuwa hivyo mpaka Imam Zaynul-Abidin (a.s.) akabadilisha mtazamo wao juu ya hilo. [46]

وكان أهل المدينة يكرهون اتخاذ أمهات الأولاد حتى نشأ فيهم علي بن الحسين بن علي، وفاق أهل المدينة فقهاً و علماً وورعاً، فرغب الناس حينئذٍ في السراري.

46. Taasisi al-Imam Zaynul Abideen, al-Sheikh Muhsin al-Huseini, Juz. 2, uk. 166.

"Na watu wa Madina walikuwa wakichukia kuwafanya watumwa mama na watoto hadi Imam Ali bin Husein (a.s.) alipoliweka bayana hilo, na akawapiku na aliwazidi watu wa Madina kifikihi, kielimu na kichamungu, basi kuanzia hapo watu wakawa wanawapenda vijakazi wao".[47]

Na hakika Imam Zainul Abidin (a.s.) alivunja mwiko wa kutofunga ndoa na vijakazi wake, naye ni mtoto wa binti ya Mtume (s.a.w.w.) na hakuna yeyote aliyemfanya duni katika nasaba na cheo, hilo ni moja ya mambo yaliyo wahamasisha wengine kuoa vijakazi wao, na pia kuzaa nao.

Muamala wa Kibinadamu wa Imam Zainul Abidin (a.s.) na Watumwa:

Mazungumzo kuhusiana na muamala wa kibinadamu wa Imam Zainul Abidin (a.s.) na watumwa yatajikita katika dondoo zifuatazo-:

1. Kuwafundisha watumwa:

Imam Zainul Abidin (a.s.) alitilia umuhimu sana suala la malezi ya watumwa katika muktadha wa dini na kitabia, na aliwafundisha hao masuala yaliyo muhimu zaidi pamoja na hukumu za kiislamu kisha baada ya hayo kuwaacha huru. Na hakika jambo hilo liliwasukuma watumwa wamtawalishe Imam Zainul Abidin (a.s.) na kubakia chini ya utawala wake na itikadi ya Ahlul-Bayt (a.s) kwa kumhami na kumtetea yeye, pia kukataa kabisa kumfanyia ubaya wowote ule.

2. Kuoa vijakazi na kuzaa nao:

Roho ya kikabila na ubaguzi na athari hasi za kijahilia zilijikita hata katika kuamiliana na watumwa na vijakazi. Lakini Imam Zainul Abidin (a.s.) alivuka vizuizi na vipingamizi vyote hivyo pamoja na mila za kiarabu zilizorithiwa kutoka katika zama za

47. Tarikh Madinatu Damishq, Ibn Asaakir, Juz. 20, uk. 57, Uyunul Akhbar, Ibn Kutaibah al-Dainuri, Juz. 4, uk. 10.

ujinga, na yeye mwenyewe alimuoa kijakazi pamoja na hadhi yake kubwa, cheo chake, elimu yake ya kina, nasaba na asili ya kiarabu. Na hakufanya hivyo isipokuwa ni ili tu athibitishe hukumu za kisharia, na malengo makubwa ya Uislamu pia kuondoa mfumo wa kitabaka na kikabila wa makosa. Na hakika ukoo wa Umayya ulijaribu kupunguza na kudunisha cheo cha Imam Zainul Abidin (a.s.) na kupunguza hadhi yake, kwa sababu tu ya yeye kumuoa kijakazi wake, isipokuwa Imam (a.s.) aliwajibu hao kwa mantiki ya Uislamu yenye nguvu ya hoja na ya wazi.

Kwa hakika wapelelezi wa Abdul-Malik bin Marwan ambao Gavana wa Madina aliwasambaza kwa lengo la kuwachunguza viongozi wa umma na vinara wake ikiwa ni pamoja na Imam Zainul Abidin (a.s.) alimtaarifu kwamba Imam Zainul Abidin (a.s.) ameoa kijakazi wake. Abdul-Malik bin Marwan alikuwa na jasusi aliyekuwa akimwandikia na kumtumia habari mbalimbali zilizotokea huko, na moja kati ya habari alizomuarifu ni kwamba Ali bin Husein (a.s.) alimuacha huru kijakazi wake na kisha akamuoa basi Abdul-Malik akamwandikia barua Ali bin Husein (a.s.) na haya ndio maandiko yake:

> "Ama baada, hakika imenifikia mimi habari ya uoaji wako wa kijakazi wako, na unajua wewe ni mkuraishi na sifa hiyo unaipeleka kwa mtoto wako, basi hapakuwa ndani ya nafsi yako mtazamo na upeo wa mbali juu ya mtoto wako".

Na Imam Ali bin Husein (a.s.) akamwandikia akimjibu jawabu lenye nguvu ya hoja, dalili na mantiki ya Uislamu, na hili hapa andiko lake:

> "Ama baada, hakika imenifikia barua yako ukinishambulia kwa kuoa mimi kijakazi wangu, unadhani katika wanawake wa kikuraishi kutokana na kusifika kwao katika ukwe na katika kuzaa yupo wa kupata naye mtoto, na kwamba hakuna aliye juu ya Mtume (s.a.w.w.) kwenye cheo wala sifa. Na hakika niliyemuoa alikuwa ni mmilikiwa wa mkono wangu wa kiume aliyetoka kwangu mimi (nilimpa uhuru) ni kama Mwenyezi

Mungu (Azza wa Jalla) alivyotaka katika jambo hili ambalo nimepata kwalo thawabu zake, kisha nikamrejesha kwa sunna (kwa ndoa) na yule aliye mwema katika dini ya Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) hawezi kuacha kitu katika amri yake, na hakika Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) ameshaondoa kupitia Uislamu ubaguzi na akahimiza upuuzwe, na akaondoa lawama basi hakuna mwislamu yeyote awezaye kulaumu, bali lawama ni ya ujahilia na sio ya Uislamu".

Na pindi aliposoma barua hiyo alimtupia mwanawe Suleiman naye akaisoma, kisha akasema: "Ewe kiongozi wa waumini! Ali bin Husein (a.s.) amekufunika kwa ufahari." Akasema:

يا بني لا تقل ذلك، فإنها ألسن بني هاشم التي تفلق الصخر وتغرف من بحر، إن علي بن الحسين يا بني يرتفع من حيث يتضع الناس.

"Usiseme hivyo ewe mwanangu, hakika hao ni wajuzi wa lugha katika ukoo wa Hashim ambao hupasua jiwe na hukata mawimbi ya bahari ewe mwanangu! Hakika Ali bin Husein daima huwa juu kadiri watu walivyo chini".[48]

Na historia inanukuu kwetu sisi mazungumzo makali baina ya Zayd bin Ali na Hisham bin Abdul-Malik Umawiy pindi Zayd bin Ali alipoingia kwa Hisham ibn Abdul-Malik, na Hisham alimkusanyia watu wa Sham na akaamrisha wabane njia ili asiweze kufika karibu yake. Basi Zayd akamwambia: "Hakika hakuna yeyote miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu aliye juu kiasi kwamba asiusiwe kumcha Mwenyezi Mungu. Wala hakuna yeyote miongoni mwa waja wake aliye chini kiasi kwamba asiusie kumcha Mwenyezi Mungu, na mimi ninakuusia ewe kiongozi wa waumini kumcha Mwenyezi Mungu".

Hisham akamwambia: Wewe unajiandalia mazingira ya kuwa

48. Furu al-Kaafiy, al-Sheikh al-Kulaini, Juz. 3, uk. 348, Namba: 4, al-Waafi, al-Faydh al-Kaashaani, Juz. 22, uk. 46, Namba: 20864. Wasail al-Shia, al-Hur al-Amili, Juz. 20, uk. 72-073, Namba: 25063.

khalifa na unataraji kuwa utaupata. Lakini kamwe hutaupata ewe usiye na mama, na hakika wewe unatokana na kijakazi"!

فقال له زيد: انى لا أعلم أحداً أعظم منزلة عند الله من نبى بعثه وهو ابن أمة، فلو كان ذلک يقصر عن منتهى غاية لم يبعث، وهو اسماعيل بن ابراهيم (ع)فالنبوة أعظم منزلة عندالله أم الخلافة يا شهام؟ وبعد فما يقصر برجل أبوه رسول الله:(ص) وهو ابن على بن أبى طالب (ع)۔

Zayd akamwambia: Hakika mimi simjui yeyote mwenye cheo na daraja mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko Nabii ambaye alitumwa naye akiwa ni mtoto wa kijakazi, na lau ingelikuwa hilo linapunguza chochote basi asingetumwa, naye ni Ismail ibn Ibrahim (a.s.) ewe Hisham! Unabii una daraja kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu au ukhalifa Na baada ya hilo basi kitu gani kitampunguzia mtu ambaye baba yake ni Mtume (s.a.w.w.) naye ni mtoto wa Ali bin Abi Twalib (a.s.)." [49]

Na ukoo wa Umayya wanazungumza kwa maneno ya kijahiliya, kwa kiasi cha kujikweza, wakati Imam Zainul Abidin (a.s.) na mwanae Zaid wanazungumza kwa maneno ya kiislamu, ambao umevunja tabia na desturi za kijahilia zenye kuchukiza.

3. Kuwa mpole kwa watumwa:

Ulisifika muamala wa Imam Zainul Abidin (a.s.) na watumwa na vijakazi kwa huruma, kusamehe, wema, unyenyekevu na usamehevu (kuwasamehe hao). Na hakika historia imesajili mambo mengi miongoni mwa visa na ushahidi mbalimbali juu ya hilo, na kati ya hayo ni:

i. Hakika mtumwa wa Ali bin Husein (a.s.) alikuwa akisimamia mradi wake, basi siku moja akaja kuangalia akakuta ndani yake ufisadi na uharibifu mkubwa, yale aliyoyaona yalimghadhibisha na kumtia majonzi, basi akamgonga kwa fimbo iliyokuwa mkononi kwake, na akajuta juu ya hilo. Na

49. Bihar al-Anwar, al-Allama al-Majlisi, Juz. 46, uk. 186-187, Namba: 52.

aliporudi nyumbani kwake alituma ujumbe wa kuitwa mtumwa wake, alipokwenda akamkuta Imam akiwa peke yake na fimbo ipo mikononi mwake, mtumwa yule akadhani kwamba Imam (a.s.) anataka kumuadhibu yeye, basi ikazidi khofu yake, basi Ali bin Husein (a.s.) akachukua fimbo yake, na akasema:

ئاهذا، قدكان منى اليک مالم يتقدم منى مثله، وكانت هفوة وزلة، فدونک السوط واقتص منى۔

"Ewe kijana! Kulikuwa na mambo niliyokutendea kutokana na kuteleza na sio kwa makusudio, basi chukua fimbo unilipizie k i s a s i." Kijana akasema: "Ewe bwana wangu! Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika mimi nilidhani unataka kuniadhibu, na mimi ni mwenye kustahiki kupata adhabu, na vipi nilipize kisasi kwako".

Akasema: "Acha hilo lipiza kisasi"

A k a s ema: "Najilinda kwa Mwenyezi Mungu, wewe upo katika nafasi na wasaa." Basi alirudia hivyo mara kadhaa, na mara zote hizo yule kijana aliitukuza kauli yake, na pindi alimuona halipizi kisasi, akamwambia:

أما إذا أبيت، فالضيعة صدقة عليك

"Kwa kuwa umekataa, basi kile kilichopotea ni sadaka kwako". Na akampatia yeye huo mradi.[50]

ii. Mmoja wa vijakazi wa Imam Ali bin Husein (a.s.) alikuwa akimwagilizia maji naye akiwa anatawadha kwa ajili ya swala, basi birika likaanguka kutoka mikononi mwake mpaka juu ya uso wa Imam, hapo Ali bin Husein (a.s.) akainua kichwa chake kumwelekea yeye. Basi kijakazi akasema: Hakika Mwenyezi Mungu aliyetukuka amesema:

وَالْكَاظِمِينَ الْغَيْظَ.

"Na wenye kuzuia ghadhabu" Akamwambia: "Hakika nimezuia ghadhabu zangu." kasema:

وَالْعَافِينَ عَنِ النَّاسِ

50. Mustadrak al-Wasail, an-Nuri al-Tabrasi, Juz. 18, uk. 288, Namba 22773, Bihar al-Anwar, al-Allama Majlisi, Juz. 46, uk. 94.

"Na wanasamehe watu." Akamwambia: Hakika nimekusamehe akasema:

وَاللهُ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

"Mwenyezi Mungu anawapenda watenda hisani" akasema : "Nenda wewe uko huru".[51]

iii. Imam Ali bin Husein (a.s.) alimwita mtumwa wake mara mbili na hakumuitikia, kisha akamwita kwa mara ya tatu, akasema: Ewe mwanangu! Hukusikia sauti yangu Akasema: Bila shaka nimeisikia.

Akasema: Kwa nini hukuniitikia Akasema: Nilikuwa nahisi nina amani kwako.

قال: الحمد لله الذى جعل مملوكى يأمننى۔

Akasema: Shukurani zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye amejaalia yule ninayemmiliki kuwa na amani nami.[52]

Kwa hakika visa hivi vinajulisha juu ya suala la kusamehe, Imam Zainul Abidin (a . s.) aliishi na watumwa wake kwa upole, kwa kusamehe, hisani na utu, hatuoni mfano wake na anayelingana naye isipokuwa babu yake bwana Mtume (s.a.w.w.) na baba zake watoharifu.

4. Kila mwaka huwaacha huru watumwa:

Imam Zainul Abidin (a.s.) alikuwa na utaratibu wa kuwaacha huru watumwa, basi alikuwa anafanya vikao vya sherehe kila mwaka ili kuwaacha huru kwa ajili ya kupata thawabu na malipo na pia kuwahamasisha wengine kuwaacha huru watumwa, na hiyo ilikuwa kwa lengo la kufanikisha uhuru wa mwanadamu, na kuondokana na hali ya utumwa.

51. Mustadrak al-Wasail, an-Nuri al-Tabrasi, Juz. 1, uk. 345. Namba: 801, Bihar al-Anwar, al-Allama Majlisi, Juz. 46, uk. 68, Namba:36.

52. Tarikh Madinatu Damishq, Ibn Asaakir, Juz. 41, uk. 387, Bihar al-Anwar, al-Allama al-Majlisi, Juz. 46, uk. 56, Namba:6.

Na hakika alikuwa Imam (a.s.) akiwajali watumwa na akiishi nao muda mrefu, kisha akiwaacha huru ili waishi wakiwa huru.

وما من سنة الا و كان يعتق فيها في آخر ليلة من شهر رمضان المبارك ما بين العشرين رأساً إلى أقل أو أكثر...

"Na hakuna mwaka isipokuwa alikuwa akiwaacha huru watumwa 20 au pungufu kidogo au zaidi, katika usiku wa mwisho wa mwezi wa Ramadhani.[53]

Na hakumtumikisha mtumishi zaidi ya uwezo wake, na alikuwa anapommiliki mtumwa mwanzoni mwa mwaka au katikati ya mwaka, na unapofikia usiku wa kuamkia Idil-Fitri huwaacha huru watumwa, hubadilisha wasiokuwa hao katika mwaka wa pili, kisha huwaacha huru, alifanya hivyo mpaka alipoaga dunia na kukutana na Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla).

Na inadhihiri kutoka katika baadhi ya hadithi kwamba Imam (a.s.) alikuwa kila mwaka akifanya sherehe kubwa ya kuwaacha huru watumwa, mosi mwishoni mwa mwezi mtukufu wa Ramadhani, pili baada ya kuisha kisimamo cha Arafa, alikuwa akiwanunua unapokaribia msimu wa Hija, na akiwaacha huru hao katika siku ya tisa ya mfunguo tatu.

Na tija ya muamala huu wa kibinadamu wa Imam Zainul Abidin (a.s.) ni kwamba hakika walipatikana wengi wenye kumuunga mkono katika masuala ya kijamii na hakika hawa walisimama na Imam katika matukio mengi mazito, kama kusimama kwao pamoja na Mapinduzi ya Mukhtari bin Abu Ubayda Thaqafi dhidi ya Bani Umayya, na kumtetea kwao Imam Zainul Abidin (a.s.) dhidi ya yule aliyejaribu kumtweza, au kumfanya duni. Na wengi miongoni mwao wakaendelea kumtawalisha Imam (a.s) na kushikamana kwao na msingi wake wa kiitikadi, dini na fikra kutokana na waliyoyaona kuhusiana na muamala wa kibinadamu ambao hakuna

53. Taasisi Imam Zaynul Abideen, Juz. 2, uk. 181.

mfano wake sehemu yoyote ile. Hakika Imam Zainul Abidin (a.s.) kulingana na muamala wake mzuri wa kibinadamu pamoja na watumwa aliweza kubadilisha maisha ya wengi wao, aliweza kuwaingiza hao na kuwawezesha kuchanganyika katika jamii za kiislamu, na akapata kutoka miongoni mwao mapenzi yao, nyoyo zao na akili zao, nguvu ya nyongeza katika nguvu ya kiislamu na wafuasi wa Ahlul-Bayt watoharifu.

IMAMU ZAINUL ABIDIN (A.S.) NA KUWAJALI MAFUKARA

Imam Ali bin Husein (a.s.) alipigiwa mfano katika uchamungu katika muamala wa kibinadamu pamoja na mafukara na masikini, na alikuwa (a.s.) ni miongoni mwa wadau wa kazi ya kujitolea na mambo ya kheri katika aina mbalimbali. Na juu ya hilo tutataja baadhi ya visa, matukio na mifano ambayo huthibitisha hilo, miongoni mwayo ni:

Muamala Wake wa Kibinadamu na Mafukara:

i. Kuwakirimu mafukara: Imam Zainul Abidin (a.s.) alikuwa akiwajali mafukara na kuchunga mapenzi yao, na hisia zao hivyo alikuwa pale anapompa kitu muombaji humbusu ili asione juu yake athari ya udhalili na haja. Na alikuwa anapojiwa na muombaji humpokea na humwambia:

مرحباً بمن يحمل زادي إلى دار الآخرة

"Karibu sana yule ambaye anabeba masurufu ya safari ya Akhera".[54]

ii. Mapenzi yake kwa mafukara: Imam Zainul Abidin (a.s.) alikuwa mwenye upole na huruma kwa mafukara na masikini, na alikuwa akipendezwa sana na kitendo cha mayatima, wenye shida na masikini ambao hawana wao njia ya kupata kipato

54. Bihar al-Anwar, Juz. 46, uk. 98, Namba: 86. al-Muntadham, Ibn al-Jauzi, Juz 6, uk. 328, Swafwa al-Swafwatu, Ibn al-Jauzi, uk. 325. Matalib al-Suul, uk. 412, Hilyatul Auliyaa, Juz. 2, uk. 418, Nafahaat Min Siratu Aimmatu Ahlul Bayt, Baaqir Sharif al-Quraishi, Darul Hadi, Qum-Iran, Chapa ya Kwanza 1424 Hijiria, uk. 183.

kuhudhuria katika meza ya chakula chake. Na alikuwa akiwatetea hao kwa mkono wake, kama alivyokuwa akiwabebea hao chakula au kuni juu ya mgongo wake mpaka milangoni mwao na kisha akiwapatia matumizi yao. Na kutokana na kuwajali mafukara na kuwafanyia upole alichukizwa na suala la kuchuma tende usiku na kutohudhuria mafukara wakati huo, na kukosa mgao wao, basi akawaambia vijana wake wakati walipochuma usiku tende:

لا تفعل، ألا تعلم أن رسول الله (ص) نهى عن الحصاد وا الجذاذ بالليل؟ وكان يقول: الضغث تعطيه من يسأل فذلك حقه يوم حصاده

"Msifanye hivyo, hamjui hakika Mtume (s.a.w.w.) alikataza kuchuma usiku na alikuwa akisema: "Ninafurahi kumpatia yule ambaye anaomba, hakika hiyo ni haki yake siku ya mavuno yake".[55]

Na alikuwa akipendezwa kuhudhuria chakula chake mayatima, wenye shida, masikini na wale wasio na njia yoyote ya kupata kipato, na alikuwa akiwapatia kwa mkono wake na yule ambaye anafamilia humbebea chakula chake, na hakuwa amekula mpaka atoe sadaka kwacho, Twai amesema:

إن علي بن الحسين (ع) كان إذا ناول الصدقة قبلها ثم ناولها

"Hakika Ali bin Husein (a.s.) alikuwa kabla hajatoa sadaka huibusu kisha huitoa".[56]

iii. Alikataza kumrudisha muombaji: Imam Zainul Abidin (a.s.) alikataza kumrudisha muombaji na kumnyima kumpatia sadaka, nalo ni kutokana na mambo mengi mabaya ambayo hupatikana kwalo, baadhi ya hayo ni kutoweka kwa neema na

---

55. Nafahat min Seerat Aimmatu Ahlul Bayt, Baaqir Sharif al-Quraishi, Darul Hadi, Qum-Iran, chapa ya Kwanza 1424 Hijiria, uk. 183.

56. Manaqib Aali Abi Talib, Ibn Shahr Aashub, Darul Adhwaa, Beirut-Lebnan, Chapa ya Pili 1412 Hijiria, Juz 4, uk. 166.

kukumbwa na mabalaa ghafla, amepokea Said bin Musayab amesema: Siku moja nilihudhuria kwa Ali bin Husein (a.s.) mpaka aliposwali swala ya adhuhuri, ghafla muombaji akaja na akagonga mlango, akasem: (a.s.).

أعطواالسائل،ولاتردواسائلاً

"Mpatieni muombaji, wala msimrudishe muombaji".[57]

Na Imam Ali bin Husein (a.s.) alitilia mkazo umuhimu wa suala hilo katika hadithi zake nyingi katika maneno yake. Hakika kumnyima fukara mwenye haja, na kutomsaidia yeye ni miongoni mwa yale ambayo hupelekea kutoweka kwa neema, na kupata ghadhabu ya Mwenyezi Mungu. Na zipo hadithi mutawatiri chungu nzima kutoka kwa Maimamu waongofu (a.s.) kuhusiana na hilo, basi hapaswi yule ambaye anapendelea kubakia neema ya Mwenyezi Mungu kwake kumrudisha muombaji au kumnyima aliyekata tamaa na fukara kwa kile ambacho kipo mkononi mwake.[58]

Kulipa Madeni:

Imam Zainul Abidin (a.s.) alijulikana kwa sifa ya utoaji na ukweli, alikuwa akiwalipia watu madeni yao yaliyofikia kiwango kikubwa, na wanahistoria wengi wanataja visa mbalimbali kuhusiana na suala hilo, baadhi ya visa hivyo ni:

Siku moja Imam Zainul Abidin (a.s.) alimtembelea Muhammad bin Usama bin Zayd akiwa anaumwa, basi akaanza kulia, Imam (a.s.) akamuuliza: Una jambo gani wewe Akasema: Nina deni, akamuuliza: Kiasi gani Akajibu: Dinar 15000 Akasema: Basi hilo ni langu mimi (ni juu yangu mimi kulilipa).[59]

---

57. Furu al-Kaafiy, Juz. 2, uk. 18, Hadith. 4. Al-Waafi, Juz. 10, uk. 411, Hadith Na: 9789. al-Wasail, Juz. 9, uk. 420, Hadith. 12379.

58. Nafahaat min Seeratu Aimmah Ahlul Bayt, Baaqir Sharif al-Quraishi, Darul Hadi, Qum-Iran, Chapa ya Kwanza 1424 Hijiria, uk. 184.

59. Manaqib Aali Abi Talib, Ibn Shahr Ashub, Juz. 4, uk. 177, Sir A'alaam an-Nublaa, Juz. 3, uk. 481. Swafa al-Swafatu, Juz. uk. 328. Hilyatul Auliyaa, Juz, uk. 421.

Hivyo ndivyo Imam Zainul Abidin (a.s.) alivyoweza kumuondolea mzigo wa deni Muhamad bin Usama kutoka mabegani mwake, na hakusimama kutoka katika kikao chake hadi alipomlipia yeye.

Kulisha Chakula Mwaka Mzima:

Miongoni mwa ukarimu wa Imam Zainul Abidin (a.s.) alikuwa akilisha watu chakula mwaka mzima kila siku huko Yathriba, na akifanya hivyo wakati wa adhuhuri nyumbani kwake.[60]

Akizihudumia Familia Mia Moja:

Miongoni mwa amali zake zilizo dhahiri ni kwamba alikuwa akisaidia familia mia moja za mafukara wa Madina, na kila familia ilikuwa na watu kadhaa.[61]

Kuwafanyia Tahfifu Mafukara:

Watu wa Madina walikuwa wakiishi hali ya kuwa hawajui maisha yao yanaendaje, na pindi alipofariki dunia Ali bin Husein (a.s.) walikosa vile ambavyo walikuwa wakivipata usiku.[62]

Na katika hadithi ya Ahmad bin Hanbal kutoka kwa Muammar kutoka kwa Shaybat bin Naamat, amesema: Hakika yeye alikuwa akiwapa chakula watu mia moja, na ikasemwa: Ilikuwa katika kila nyumba kuna jumuiya ya watu. Na katika kitabu Hilyat imetajwa kwamba: Hakika Aisha aliwasikia watu wa Madina wakisema: Hatukukosa sadaka ya siri mpaka alipoaga dunia Ali bin Husein.[63]

Na Dhahabi ametaja kutoka kwa baadhi yao, hakika hao walikuwa wakisema: Hatukuikosa sadaka ya siri mpaka alipofariki Ali bin Husein. [64]

---

60. Nafahat min Seeratu Aimmah Ahlul Bayt, uk. 182.

61. Manaqib Aali Abi Talib, Ibn Shahr Aashub, Juz. 4, uk. 166. Seer A'alaam an-Nablaa, Juz. 3, uk. 481. Hilyatul Auliyaa, Juz. 2, uk. 416.

62. Swafa al-Swafaatu, Ibn al-Jauzi, al-Maktaba al-Asriyya, Beirut, Chapa ya mwaka 1430 Hijiria- 2009 Miladia, Juz. 1, uk. 326.

63. Manaqib Aali Abi Talib, Ibn Shahr Aashub, Juz. 4, uk. 166. Swafa al-Swafaatu, Ibn al-Jauzi, Juz. 1, uk. 326.

64. Siyar Aalaam Nubalaae, Juz. 3, uk. 481. Hilyatul Auliyaa, Juz. 2, uk. 417.

Na katika hadithi ya Muhammad bin Is'haq imesemwa: Hakika yeye alikuwa katika mji wa Madina na nyumba kadhaa wakadha akiwapelekea riziki yao na vile walivyokuwa wakivihitajia kwake. Hawakujua aliyekuwa akiwaletea hao na ni kutoka wapi, na alipofariki Zaynul–Abidina wakayakosa hayo basi wakapiga ukulele mmoja mkubwa.

Na katika hadithi iliyopokewa kutoka kwa Abu Ja'far (a.s.) ni kwamba alisema: "Hakika yeye alikuwa akitoka usiku wa giza na akibeba mzigo mgongoni kwake akienda mlangoni na akiugonga kisha akimpatia aliyetoka, na alikuwa akifunika uso wake pale anapompatia kitu fukara ili asimjue".

Na katika habari nyingine imetajwa kwamba: Alikuwa usiku unapoingia na macho kulala, husimama nyumbani kwake na hukusanya vile vilivyobakia kutokana na chakula cha familia yake, huviweka katika kiroba, kisha hujitwisha mabegani mwake na kutoka kuelekea nyumba za mafukara. Wengi wao walikuwa wakisimama milangoni mwao wakimngojea, na wanapomuona huonesha bishara njema kwake, na husema: Amekuja mwenye mzigo.[65]

Na imepokewa kutoka kwa Ibn Uyayna kutoka kwa Abu Hamza Thumali kwamba, hakika Ali bin Husein alikuwa akibeba mikate usiku mgongoni kwake na akiwafuata masikini gizani na akisema: Hakika swadaka katika usiku wa giza inazima ghadhabu ya Mola Mlezi,[66] na amepokea Abu Naim Isfahani na ni hili hapa andiko lake: Hakika sadaka ya siri inazima ghadhabu ya Mola Mlezi (Azza wa Jalla). [67]

Na kutoka kwa Muhammad bin Is'haq amesema: "Walikuwa watumwa wa Madina wakiishi maisha yao hali hawajui maisha yao yanaendaje, na alipofariki Ali bin Husein wakamkosa yule aliyekuwa akiwaletea usiku".

65. Manaqib Aali Abi Talib, Ibn Shahr Aashub, Juz. 4, uk. 166.
66. Siyar Aalaam Nubalaae, Juz 2, uk. 416.
67. Hilyatul Auliyaa, Juz. 2, uk. 416.

Na kutoka kwa Jarir bin Abdu–Hamid, kutoka kwa Amru bin Thabit amesema: "Pindi alipofariki Ali bin Husein (a.s.) walikuta mgongoni kwake athari mbaya katika mwili wake, kwa sababu alikuwa akibeba mizigo usiku kwenda katika nyumba za wajane".[68]

Zahri anasema: "Pindi alipoaga dunia Zaynul-Abidina (a . s.) w a k a m u o s h a, hapo wakakuta mgongoni mwake kuna mahali pameweka nundu, basi ikanifikia habari mimi kwamba yeye alikuwa akibeba usiku misaada na kuwapelekea majirani zake wasio na uwezo".[69]

Amru bin Thabit amesema: Pindi alipofariki Ali bin Husein (a.s.) walipomuosha walikuta athari nyeusi wakawa wanaangalia mgongoni kwake wakasema ni nini I k a s e m w a: Alikuwa akibeba mizigo ya unga usiku mgongoni kwake na akiwapatia mafukara. Na katika hadithi za maswahiba zetu imesemwa: Pindi alipowekwa sehemu ya kuoshea, wakaangalia mgongoni kwake wakaona nundu mfano wa nundu la ngamia kutokana na mizigo aliyokuwa akiibeba mgongoni mwake akiipeleka kwenye majumba ya mafukara.

Na hili linaonesha tabia ya kujitolea ya kivitendo ya Imam Zainul Abidin (a.s.) katika kiwango cha juu cha unyenyekevu katika muamala wake wa kibinadamu na mafukara. Na hakuna maudhi au ubaya wowote, basi ametupatia sisi masomo yenye mazingatio katika suala la kitabia na matendo ya kujitolea ambayo ni juu yetu sisi kuitekeleza kivitendo tabia hii pale tunapofanya matendo ya kujitolea katika kuwasaidia mafukara, na kuifanya jamii ikulie katika hilo na iwe na maendeleo.

IMAM ZAINUL ABIDIN (A.S.) NA WARAKA WA HAKI

Imam Zainul Abidin (a.s.) ameacha athari ya kielimu muhimu sana kwa vizazi vyote, nayo ni risala ya haki, na risala hii adhimu

68. Siyar Aalaam Nubalaae, Juz. 3, uk. 481.
69. Manaqib Aali Abi Talib, Ibn Shahr Aashub, Juz. 4, uk. 167. Hilyatul al-Auliyaa, Juz. 2, uk. 417.

ambayo Imam (a . s.) anaelezea ndani yake haki muhimu na za msingi za watu na utamaduni wa haki. Alifanya hivyo kabla ulimwengu haujazungumzia makubaliano na azimio la tangazo la ulimwengu hujatoa tangazo rasmi la haki za binadamu mwaka 1948A.D. Alifanya hivyo mamia ya miaka kabla, jambo ambalo latupatia sisi mtazamo wa kina wa wazi wa Imam Zainul Abidin (a.s.) kuhusiana na haki za binadamu.

Na waraka huu wa haki wa Imam Zainul Abidin (a.s.) huhesabiwa kuwa ni miongoni mwa athari muhimu za kielimu ambazo zimetufikia sisi baada ya Sahifat Sajjadiya, ambapo Imam (a. s.) humo anabainisha ndani yake wajibu wa binadamu kumwelekea Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) kuelekea nafsi yake na kuwaelekea viumbe wenzake. Na hakika waraka huo ameutaja Ibn Shuubat Harrani katika kitabu chake Tuhaful–Uquul, nao ni ibara ya haki 50 ,na kwa mujibu wa riwaya ya Sheikh Saduq katika kitabu chake Al–Khiswal ni haki 51.

Imam Zainul Abidin (a.s.) na Kuasisi Haki za Binadamu:

Hakika Imam Zainul Abidin (a.s.) huhesabiwa ni mwasisi wa utamaduni wa haki za binadamu, basi yeye ni wa mwanzo aliyeweka risala ya haki za binadamu kabla ya karne 14 zilizopita, na hilo ni kwa kutambua kwake umuhimu mkubwa zaidi wa kuheshimu haki za binadamu. Na hakika hiyo hutengeneza jengo la nidhamu ya kijamii yenye kushikamana na kuhakiki uwepo wa uadilifu katika jamii, kutoa dhamana ya usalama wa mahusiano ya mtu mmoja na jamii katika hali ya heshima ya kubadilishana, na kusameheana na kukubali rai ya mpinzani (mwenye kuhitilafiana naye.).

Ni muhimu sana kuingiza mada inayohusiana na suala la haki za binadamu katika mifumo ya taaluma na hivyo ni kueneza utamaduni wa haki baina ya wanafunzi na ile athari chanya inayoweza kupatikana katika silka ya mtu mmoja mmoja na kijamii kwa jumla. Ama kukosekana utamaduni wa haki za

binadamu kunapelekea kuenea kwa ubaguzi, jazba na kupituka m i p a k a, wakati kujua haki za dhati sembuse kuhusu haki za wengine hupelekea kuongoza kanuni na kukua utamaduni wa kumheshimu na kumtukuza binadamu, pia kuitendea kazi kauli yake:

وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِّنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا

"Hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini na tumewaruzuku vitu vizuri na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba".[70]

Basi Aya tukufu inaelezea utukufu wa binadamu ikifumbia macho suala la dini yake au madhehebu yake au utaifa wake au rangi yake na ukoo wake "Hakika tumewatukuza wanaadamu na tumewabeba nchi kavu na baharini na tumewaruzuku vitu vizuri na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tuliowaumba".

Hakika Imam Ali bin Husein (a . s.) aliwabainishia watu haki za mtu baada ya tukio la Twaffi ambalo limevunja haki za msingi za binadamu achilia mbali mafunzo ya Uislamu na hukumu zake.

Mambo Muhimu Yaliyomo Katika Waraka wa Haki:

Unakuja umuhimu wa Waraka wa Haki wa Imam Zainul Abidin (a.s.) kwa kuzingatia kwamba ndio mkataba wa kale zaidi kuhusu haki za binadamu, kwani mkataba wa kimataifa wa haki za binadamu tangu ulipotangazwa umri wake hauzidi karne mbili . Kwani kwa mujibu wa jamii ya kimataifa ni kwamba haki muhimu zaidi ni zile zilizoelezwa na mikataba mbalimbali kuhusiana na haki za binadamu, na tangazo la ulimwengu la haki za binadamu lililotolewa na Umoja wa Mataifa tarehe 10/12/1948, ndio mkataba muhimu wa haki za binadamu, tangazo hili ambalo limeambatana na kanuni zake lilitokana na tangazo la Mapinduzi ya Ufaransa

70. Surat Bani Israil: 17:70.

ambayo yalitokea mwaka 1789 A D na humo limezitambua haki za binadamu na kukiri haki za msingi za mtu mmoja mmoja.

Hakika Waraka wa Haki wa Imam Sajjad (a . s.) w e n y e w e umeelezea haki nyingi zaidi kuliko zile zilizoandikwa katika tangazo la ulimwengu la haki za binadamu, ni Waraka wa Haki 50, na katika riwaya nyingine haki 51. Na amezitaja hizo mwandishi wa kitabu Tuhaful-Uquul, nazo zinafikia haki 50 na kwa riwaya ya Sheikh Saduq katika kitabu chake Al-khiswal zipo haki 51. Tangazo la ulimwengu la haki za binadamu lenyewe halina zaidi ya 29. Aidha Waraka wa Haki wa Imam (a . s.) umetaja haki ambazo mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu imejifanya kutozitambua kama vile haki ya Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) kwa mja wake, nayo ndiyo haki kubwa zaidi, bali ndio asili na msingi wa haki zote.

Kisha Imam Zainul Abidin (a.s.) akaelezea haki za binadamu ambazo zimefaradhishwa na Mwenyezi Mungu kumwelekea binadamu mwenyewe, na aina ya mahusiano ya binadamu katika nafsi yake kutokana na mtazamo wa Uislamu.

Haki Zilizo Muhimu Zaidi:

Imam Zainul Abidin (a.s.) amebainisha katika Waraka wa Haki wajibu wa mtu mbele ya Allah, na mbele ya nafsi yake na mbele ya viumbe wenzake, na hivyo inawezekana kuzigawanya haki za msingi za binadamu ambazo Imam Zainul Abidin (a.s.) kaziwasilisha katika waraka wake kama ifuatavyo:

1. Haki ya muumba na haki ya kiumbe.
2. Haki za viungo

Nazo zipo kama ifuatavyo haki ya ulimi, haki ya masikio, haki ya macho, haki ya mkono, haki ya mguu, haki ya tumbo na haki ya viungo vya uzazi.

3. Haki ya matendo

Nazo ni haki zifuatazo Haki ya swala, haki ya Hija, haki ya funga, haki ya sadaka na haki ya zawadi.

4. Haki ya maimamu

Haki hizo ni kama zifuatazo Haki ya sultan, haki ya yule anayekufundisha elimu, haki ya kiongozi wako, na haki ya mfalme.

5. Haki za raia:

Haki za raia nazo zimegawanyika katika makundi yafuatayo haki ya raia kwa kiongozi, haki ya raia katika elimu, haki ya mke, haki ya anayemilikiwa.

6. Haki za ndugu

Na haki za ndugu zipo katika makundi yafuatayo Haki ya mama, haki ya baba, haki ya mtoto, haki ya kaka (au mdogo) haki ya yule anayekuneemesha, haki ya yule uliyemneemesha.

7. Haki za watu wote na vitu

Zipo haki 29 nazo ni haki ya mwadhini, haki ya Imam wa swala ya jamaa, haki ya yule aliyekaa nawe, haki ya sahiba, haki ya mshirika, haki ya mkubwa, haki ya mdogo, haki ya Waislamu, haki ya watu wa dhima.....na haki nyinginezo.

Na hapa tunaona kwamba Imam Zainul Abidin (a.s.) alihitimisha Waraka wake wa haki mbalimbali kwa kutaja haki za Waislamu na hata ikiwa wametofautiana katika madhehebu yao, rai zao, na marejeo yao ya kifikra, basi kila mwislamu atekeleze ibada zake, kauli zake na yale anayoitikadi au itikadi zake kulingana na madhehebu yake.

Kisha kutekeleza haki za yule anayeshirikiana naye katika ubinadamu, katika nchi moja, na nidhamu moja ya kisiasa, hata kama watatofautiana katika dini, lakini wao wanashirikiana katika ubinadamu, na mfumo mmoja wa kisiasa, basi wao wana haki za

uraia na wana uhuru wa kufanya mambo yao ya kidini, bila kuingiliwa. Na wanao uhuru wa kufanya mambo yao ya kiibada, kama vile walivyo na haki ya kutenda kulingana na sharia zao katika ndoa zao na talaka zao, na mengineyo yanayohusiana na hali za mtu binafsi, Imam Zainul Abidin (a.s.) amesema:

وحق أهل الذمة: أن تقبل منهم ما قبل الله عزوجل، ولا تظلمهم ما وفوالله عزوجل بعهده

"Na haki ya watu wa dhima (wasiokuwa waislamu) ni ukubali kutoka kwao yale ambayo Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) ameyakubali, usiwadhulumu hao yale ambayo wamemtekelezea Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) katika ahadi yake".[71]

Na waraka huu unatengeneza agano madhubuti na mkataba imara wa kihistoria kutokana na umuhimu wake mkubwa, nao unahitajika kusomwa zaidi na kufanyiwa upembuzi yakinifu, na ndani yake kuna dalili ya kina juu ya yale yaliyotangulia katika fikra ya Ahlul-Bayt na mfumo wao wa kiungu.

Waraka wa Haki na Uadilifu wa Kijamii:

Kwa hakika kupangilia mahusiano ya kijamii juu ya msingi wa kuainisha mkusanyiko wa haki kwa undani, ndio kipaumbele cha kwanza cha mpangilio wa jamii ya kiislamu, nacho ndio msingi wa kukubalika kiakili sharia zote za kiislamu, hivyo yule ambaye ataufahamu kwa undani waraka huu na akasoma kwa makini haki za muumbaji na haki za viumbe baadhi yao kwa baadhi, ataweza kufahamu siri za sharia za kiislamu na falsafa ya hukumu ambazo zimeletwa na sharia za kiislamu ili kupangilia uhai wa binadamu mmoja mmoja na jamii.

Hakika uadilifu wa jamii au wa kiuchumi au wa kiidara hautapatikana maadamu haujafanyiwa kazi mpango wa haki kwa undani kwanza, na kupangilia hukumu na sharia mbalimbali juu ya

71. al-Waafi, Al-Faidh al-Kaashani, Juz. 6, uk. 134, (Mlango wa Ufafanuzi wa Haki ya kila mwenye Haki.)

msingi wa haki hizo. Na tulijualo ni kwamba hakika Imam amewatangulia wasomi na watunga kanuni wote katika ulimwengu wa kiislamu bali katika ulimwengu wa binadamu katika mchakato huu ambao juu ya msingi wake inajikita misingi au mizizi ya tabia na malezi na mpangilio wa kijamii.

Na kabla Imam hajabainisha haki mbalimbali anatoa maelezo kwamba zipo haki zenye kuzungumzia binadamu na hapana budi yeye kuzijua hizo. kisha anabainisha haki kubwa zaidi nayo ni ile inayomfungamanisha Mwenyezi Mungu (Azza wa Jalla) na mja w a k e, kisha anatanzua kutoka humo haki za binadamu zilizofaradhishwa na Mwenyezi Mungu kumwelekea binadamu m w e n y e w e, basi anabainisha mahusiano mbalimbali ya mwanadamu katika nafsi yake kulingana na maelekezo ya Mungu. Kisha anamalizia aina ya mahusiano kati ya binadamu na jamii yake ambayo yanafungamana na viongozi na raia, na wachungaji na wanaochungwa pamoja na kubainisha aina ya maimamu na maamuma na daraja zao. Kisha anabainisha mahusiano mengine pamoja na ndugu, familia na wahusika wake, kisha wale wanaokuwemo katika familia kutokana na watumwa na vijakazi. Kisha haki nyingine kama vile haki ya mwadhini na Imam katika swala, unayekaa naye unayeshirikiana naye (mshirika) mdaiwa, mgomvi wako, muomba nasaha, mnasihi, muombaji, muombwa, mdogo na mkubwa.....hadi anaishia kwa yule anayeshirikiana naye katika ubinadamu, katika dini yake miongoni mwa wanadamu, kisha haki za mtu na yule anayeshirikiana naye katika ubinadamu, na katika mfumo wa kisiasa ambao anaunyenyekea huo hata kama akiwa sio watu wa mila yake na dini yake.

Na ni juu yetu tufaidike na Waraka wa Haki wa Imam Zainul Abidin (a.s.) na tulipe umuhimu mkubwa zaidi suala la haki za binadamu na tufanye kitu kinachowezekana ili kueneza utamaduni wa haki baina ya watu, mpaka kila mtu ajue haki zake na wajibu wake mmoja mmoja, kijamii na kiuchumi kwa kiasi cha kuweza kuleta uadilifu wa kijamii kwa viumbe wote.

Shukurani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa walimwengu. Kisha rehema za Mwenyezi Mungu na amani zimfikie Mtume Muhammad pamoja na ndugu zake watoharifu.

REJEA

1. Qur'an tukufu.
2. Al-Kamil fi Tarekh cha Ibn Athir Abul–Hasan Ali bin Abi Karam Muhammad bin Muhammad bin Abdul-Karim bin Abdul–Wahid Shaybani (amefariki 630 Hijiria) amepitia na kukifanyia masahihisho Muhammad Yusuf Riqaa, kimeshapishwa na Darul–Kutubil Ilmiyya, chapa ya Beirut Lebanon, toleo la nne 1424 Hijiria / 2003 A.D.
3. Al-Muntadham fi Tarikh Umamu wal-Muluk cha Ibn Jawzi, Abu Faraj Abdul–Rahman bin Ali bin Muhammad (amefariki 597 Hijiria, kimechapishwa na Darul-Kutubil-Ilmiyya, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1412 Hijiria / 1992 A.D.
4. Sifat Swafwat cha Ibn Jawzi, Abu faraj Abdul-Rahman bin Ali bin Muhammad (amefariki 597 Hijiria, Kimehakikiwa kimehakikiwa na Dr. Abdul-Hamid Indawi, kimepigwa chapa na maktabatul–Asriyya, Beirut. Lebanon, toleo la mwaka 1430 Hijiria / 2009 A.D.
5. Uyunul–Akhbari cha Ibn Qutayba Daynury Abu Muhammad Abdullah bin Abdul-Majid bin Muslim (amefariki 276 Hijiria / 889 A.D. kimepigwa chapa na Darul–Kutubil Ilmiyya, Beirut, toleo la tatu 1423 Hijiria / 2003 A.D.
6. Tuhaful-Uquul An Aali Rasul cha Ibn Shaybat Al-Harrani, Abu Muhammad Hasan bin Ali bin Husein, amekifanyia masahihisho na kuweka mstari wa pambizo Ali Akbar Ghaffari, kimepigwa chapa na Muassasat Nashri Islamiyya, Qum, toleo la pili 1404 Hijiria.
7. Manhaj Da'wat wa Manhajul–ibadaat cha Ibh Taus, Abul–Qasim Ali bin Musa bin Ja'far bin Muhammad (amefariki

6 6 4 Hijiria) kimechapishwa na Muassasat Al-Aalamiy ya uchapishaji, Beirut–Lebanon toleo la tatu 1432 Hijiria / 2011 A.D.
8. Tarikh Madinat Damishaqi cha Ibn Asakir, Abul–Qasim Ali bin Hasan bin Hibatullah bin Asakir Damishaqi (amefariki 1176 A.D.) kimechapishwa cha Darul–Fikri, Beirut Lebanon, toleo la mwaka 1415 Hijiria.
9. Hilyatui–Awliya wa Twabatul-Asfiyaa cha Al–Isbahani, Abu Naim Ahmad bin Abdillah bin Ahmad bin Is-haq bin Musa (amefariki 430 Hijiria / 1038 A.D. kimehakikiwa na Saami Abu Jahiin, kimechapishwa na Darul-Hadith, Cairo. Misri, 1430 Hijiria / 2009 A.D.
10. Siirat Aimmat Ithna Ashar cha Al–Biishawani Mahdi, kimepigwa chapa na Darul-Kutubi Arabi, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1426 Hijiria / 2005 A.D.
11. Tafswiil Wasail Shiia ila Tahswiil Masail shariiat cha Al–Hurru Amily, Abu Ja'far Muhammad bin Hasan bin Ali (amefariki 1104 Hijiria, kimepigwa chapa na Muassasat Aalul-Bayt Li ihyai Turath, Beirut Lebanon, toleo la kwanza 1413 Hijiria / 1993 A.D.
12. Mausuat Imam Zainul-Abidin (a.s.) cha Al-Husein Muhsin, kimepigwa chapa na Darul-Mahajjatul-Baidhai, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1435 Hijiria.
13. Sayru Aalam Nubalaai cha Ad-dhahabi, Shamsu Diin Muhammad bin Ahmad bin Uthman (amefariki 784 Hijiria), kimepigwa chapa na Maktabut Al-riya, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1435 Hijiria / 2014 A.D.
14. Mizanul-Hikmat cha Al–Ray Shahri cha Muhammad, kimepigwa chapa na Muassasat Darul-Hadith Thaqafiya, Beirut Lebanon, toleo la pili 1419 Hijiria.
15. Sahifatul-Sajjadiya Al-Kamilat cha Zaynul–Abidina Imam Ali bin Husein bin Ali bin Abi Twalib (a.s.) (amefariki 95 Hijiria), kimepigwa chapa na Muassasat Aalamiy ya uchapishaji, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1424 Hijria / 2003 A.D.
16. Nahjul-Balagha cha Imam Ali bin Abi Twalib, kimekusanywa

na Sharifu Ridhawi, Abul-Hasan Muhammad bin Abi Ahmad Husein bin Musa Ibn Muhammad bin Musa bin Ibrahim ibn Imam Musa Al-Kadhim (amefariki 406 Hijiria / 1015 A.D. Sharhu ya Sheikh Muhammad Abdih, kimepigwa chapa na Darul–Balagha, Beirut. Lebanon, toleo la nne 1409 Hijiria, 1989 A.D.

17. Al-Aamaly cha Sheikh Saduq, Abu Ja'far Muhammad bin Ali bin Husein bin Babaway Al-Qummi (amefariki 481 Hijiria / kimepigwa chapa na Muassasatul–Bi'that Qum, toleo la kwanza 1417 Hijiria.

18. Al–Khiswal cha Sheikh Saduq, Abu Ja'far Muhammad bin Ali bin Husein bin Babaway Al-Qummi (amekufa mwaka 381Hijiria), kimepigwa chapa na Muassasatul-Aalamiy ya uchapishaji, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1410 Hijiria / 1990 A.D.

19. Mustadrakul-Masail cha Mirza Husein bin Muhammad Taqii bin Ali Muhammad bin Taqi Nuriy (amefariki 1320 Hijiria), kimepigwa chapa na Darul-Hidaya, Beirut – Lebanon, toleo la tano 1412 Hijiria / 1991 A.D.

20. Majmaul-Bayan fi Tafsiril-Qur'an cha Abu Ali Fadhli bin Hasan Twabarasi (amefariki 548 Hijiria), kimepigwa chapa na Darul-Maarifat, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1406 Hijiria / 1986 A.D.

21. Tarikh Twabary Tarikh Umamu wal-Muluk cha Abu Ja'far Muhammad bin Jarir bin Yazid bin kathir bin Ghalib Twabari (amefariki 310 Hijiria / 923 A.D.), kimepigwa chapa na Darul-Kutubil-ilmiyya, Beirut–Lebanon, toleo la pili 1424 Hijiria / 2003 A.D.

22. Kitabul-Waafi cha Al-Faydh Kashani, Muhammad bin Murtadha (amekufa 1019 Hijiria), kimehakikiwa na Sayyid Ali Abdul-Muhsin Bahrul-Ulumi, kimepigwa chapa na Darul–Ihya Turath Arabi, Beirut–Lebanon, toleo la kwanza 1433 Hijiria / 2011A.D.

23. Nafahal Min Siirat Aimmat Ahlul-Bayt (a.s.) cha Al-Qurashi Baqir Sharif, kimepigwa chapa na Darul-Huda Qum, toleo la kwanza 1424 Hijiria.

24. Usulul-Kaafi cha Muhammad bin Yakub Al-Kulayni

(amekufa 329 Hijiria), amekiwekea irabu, kukifanyia masahihisho na kuweka mstari wa pambizo Sheikh Muhammad Ja'far Shamsu Diin, kimepigwa chapa na Darul-Taa'rif cha uchapishaji, BeirutLebanon, toleo la 1419 Hijiria / 1996 A.D.

25. Furuu Kaafi cha Muhammad bin Yakub Al-Kulayn i (amekufa 329 Hijiria), ameweka irabu, kukifanyia masahihisho na kuweka mstari wa pambizo Sheikh Muhammad Ja'far Shamsu Diin, kimepigwa chapa na Darul-Taa'rif ya uchapaji, Beirut Lebanon, toleo la mwaka 1413 Hijiria / 1992 A.D.

26. Kanzul-Ummal fi Sunanil-Aqwal wal Af'aal cha Al-Muttaqi Hindi, Alau Diin Ali bin Hassam Diin (amekufa 975 Hijiria / 1567 A.D.), kimepigwa chapa na Muassasatul-Risalat, Beirut Lebanon, toleo la mwaka 1409 Hijiria / 1089 A.D.

27. Biharul-Anwar li Duraril-Akhbar Aimmatil-Al At-har cha Muhammad Baqir bin Muhammad Taqii Al-Majlisi (amekufa 1111 A.D.), kimepigwa chapa na Muassasatul-Ahlu-Bayt Qum, toleo la nne 1409 Hijiria / 1989 A.D.

BACK COVER

Hakika Imam Ali bin Husain Zainul Abidin, maarufu pia kwa jina la Imam Sajjad (a.s.) alidhihiri katika kipindi cha Uimamu wake kama Imam wa Waislamu, na ambaye watu walikuwa wanarejea kwake katika masuala ya kidini, na hivyo alikuwa mnara wa elimu, mbainifu wa hukumu za kisharia na mfasiri wa Qur'ani Tukufu.

Alikuwa mfano wa kuigwa wa hali ya juu katika ibada, kujinyima, takwa, na uchamungu, mpaka akawa anaitwa: mwingi wa kusujudu, pambo la wenye kuabudu na Imam wa wachamungu.

Kwa hakika Imam Zainul Abidin (a.s) katika uhai wake alikabiliwa na changamoto nyingi na mambo makubwa ya kumtia majonzi, na kubwa zaidi lilikuwa ni tukio la Karbala lenye kuhuzunisha na kuumiza mno. Yale yaliyofuatia baada ya tukio hilo ambayo yalimfanya Imam Zainul Abidin (a.s.) aishi katika kipindi kigumu,

na alikabiliana nayo kwa subira, kujitenga na hekima.

Kwa hakika, Imam Zainul Abidin (a.s.) alichukua majukumu ya Uimamu baada ya kufa shahidi baba yake Imam Husain (a.s.) Kilikuwa ni kipindi kigumu katika nusu ya pili ya karne ya kwanza ya Hijria, na akatekeleza jukumu lake la uongozi na dini pamoja na kuwa mazingira hayakuwa rafiki kwake na yalikuwa magumu mno.

Imam Zainul Abidin (a.s.) aliona Umma unakabiliwa na hatari kubwa, na iliyodhihirika zaidi ni yale yaliyoleta athari mbaya kutokana na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali zilizoletwa ambazo zilileta athari katika shakhsia ya Mwislamu, na mwelekeo wa Umma wa Kiislamu.

Jambo lingine ni mmomonyoko wa kidini na kitabia, na kuenea maovu na mambo ya haramu ambayo ni matokeo ya maisha ya anasa na ubadhirifu katika kuendekeza starehe za dunia na matamanio yake. Hayo, na yanayofanana na hayo yaliwafanya watu washughulike na dunia zaidi na kuwaweka mbali na roho ya Uislamu na makusudio yake, na malengo yake makubwa.

Baada ya matukio ya kuhuzunisha ya Karbala, Imam Zainul Abidin (a.s.) alianza kutilia umuhimu suala la kumjenga binadamu na kumlea kwa malezi madhubuti ya kidini na kielimu kwa ajili ya kuandaa watu na wadau wa ujumbe ambao wataongoza Umma na kusahihisha mwenendo wa makosa, pia kuchangia katika kueneza elimu na maarifa katika nyanja mbalimbali za kielimu.

Kitabu hiki kinaangazia kwa muhtasari baadhi ya mambo ambayo Imam Zainul Abidin (a.s.) aliyasimamia, yakiwa ni mambo muhimu katika mchakato wa kumjenga mwanadamu katika nyanja za kiroho, kiuchumi, ubinadamu na haki.

Imam Zainul Abidin (a.s.) na Kumjenga Binadamu

Hakika Imam Ali bin Husain Zainul Abidin, maarufu pia kwa jina la Imam Sajjad (a.s.), alidhihiri katika kipindi cha Uimamu wake kama Imam wa Waislamu, na ambaye watu walikuwa wanarejea kwake katika masuala ya kidini, na hivyo alikuwa mnara wa elimu, mbainifu wa hukumu za kisharia na mfasiri wa Qur'ani Tukufu.

Alikuwa mfano wa kuigwa wa hali ya juu katika ibada, kujinyima, takwa, na uchamungu, mpaka akawa anaitwa: mwingi wa kusujudu, pambo la wenye kuabudu na Imam wa wachamungu.

Kwa hakika Imam Sajjad (a.s.) katika uhai wake alikabiliwa na changamoto nyingi na mambo makubwa ya kumtia majonzi, na kubwa zaidi lilikuwa ni tukio la Karbala lenye kuhuzunisha na kuumiza mno. Yale yaliyofuatia baada ya tukio hilo ambayo yalimfanya Imam Sajjad (a.s.) aishi katika kipindi kigumu, na alikabiliana nayo kwa subira, kijitenga na hekima.

Kwa hakika, Imam Sajjad (a.s.) alichukua majukumu ya Uimamu baada ya kufa shahidi baba yake Imam Husain (a.s.).

Kilikuwa ni kipindi kigumu katika nusu ya pili ya karne ya kwanza ya Hijria, na akatekeleza jukumu lake la uongozi na dini pamoja na kuwa mazingira hayakuwa rafiki kwake na yalikuwa magumu mno.

Imam Sajjad (a.s.) aliona Umma unakabiliwa na hatari kubwa, na iliyodhihirika zaidi ni yale yaliyoleta athari mbaya kutokana na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali zilizoletwa ambazo zilileta athari katika shakhsia ya Mwislamu, na mwelekeo wa Umma wa Kiislamu.

Jambo lingine ni mmomonyoko wa kidini na kitabia, na kuenea maovu na mambo ya haramu ambayo ni matokeo ya maisha ya anasa na ubadhirifu katika kuendekeza starehe za dunia na matamanio yake. Hayo, na yanayofanana na hayo yaliwafanya watu washughulike na dunia zaidi na kuwaweka mbali na roho ya Uislamu na makusudio yake, na malengo yake makubwa.

Baada ya matukio ya kuhuzunisha ya Karbala, Imam Sajjad (a.s.) alianza kutilia umuhimu suala la kumjenga binadamu na kumlea kwa malezi madhubuti ya kidini na kielimu kwa ajili ya kuandaa watu na wadau wa ujumbe ambao wataongoza Umma na kusahihisha mwenendo wa makosa, pia kuchangia katika kueneza elimu na maarifa katika nyanja mbalimbali za kielimu.

Kitabu hiki kinaangazia kwa muhtasari baadhi ya mambo ambayo Imam Zainul Abidin (a.s.) aliyasimamia, yakiwa ni mambo muhimu katika mchakato wa kumjenga mwanadamu katika nyanja za kiroho, kiuchumi, ubinadamu na haki.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
SMS: +255 778 300 140
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibnrtv.co.tz
Vitabu mtandaoni: www.alitrah.info/ebooks/

ISBN 978-9987171408-8
9 789987 171408